# Nipashe

Ijumaa Oktoba 25, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580058

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

…dian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Wasafirishaji wahamiaji haramu wabadili mbinu kuwakwepa polisi

UKURASA 3



Ukurasa 15

Kipunguni Dar waja na mkaa wa maboksi

Ukurasa 14

Tija kiuchumi: Matumizi 'simu janja' yanashika nafasi gani katika uzalishaji?

BUFE

Ijumaa Oktoba 25, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 20

'Shida ya vijana wazito kukubali mabadiliko ya kuwatoa walipo'

Orodha changamoto zinazoumiza wakulima pamba Kanda ya Ziwa

Na Sabato Kasika

KUPOROMOKA bei ya pamba katika soko la dunia, kunaelezwa kumeyumbisha wakulima na kusababisha baadhi yao kukataa tamaa na kujipanga kulima mazao mengine ya biashara.

Hilo lipo kukiwapo hitaji kwamba wakulima wa zao hilo nchini wanahitaji mazingira ya kuwakizia mapato yao kupitia uzalishaji wenye tija shambani hadi sokoni, ili waondokane na kutegemea huruma ya ongezeko la bei katika soko la dunia. Uingiliaji wa kimkakati wa juu ndio unaoweza kutatua mgogoro wa kuanguka bei kwa muda mfupi na mrefu, ili kutojirudia vikwazo kila mara na utaendeleza ushindani wa pamba kwa ajili ya viwanda vya ndani na vya nje.

MADIWANI

Diwani wa Kata ya Matongo, wilayani Meatu, Ng'adida Tuyi, anasema pamba ni kimbilio la wakulima wao ambao baada ya mavuno matarajio yao ni kununua mifugo na mashamba.

INAENDELEA UK.18

UCHUMI

Habari katika picha

Ukurasa 17

Mradi unaozuia ng'ombe kufa, huwanenepesha, majosho kibao Ukurasa 16

UKURASA 13

# Vikwazo 12 ufanyaji biashara vyaanikwa

• **Ni Ripoti** ya WB yataja kodi na vibali, Tanzania yaelezwa kuwa ya 141 kati ya 190 kwenye ubora... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 5

**ACT-WAZALENDO YAKUBALIWA KESI TAFSIRI UKOMO WA URAIS**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imekubali ombi la Chama...

UKURASA WA 10

**HAKIMU AKWAMISHA KESI YA KABENDERA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepiga kalenda...


## Rugemalira adaiwa kuugua mahabusu

UKURASA 3



Baadhi ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita wa Shule ya Sekondari Kiwanja wilayani Chunya, Mkoa wa Mbeya, waliosimamishwa, wakirejea shuleni jana, baada ya kukamilisha taratibu walizopewa na Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila. **PICHA: NEBART MSOKWA**


Scan Hapa



Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Wamiliki malori waonywa bila EFD hakuna leseni

UKURASA 2


MICHEZO SAMATTA AWAAMSHA WACHAMBUZI ENGLAND UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# Mvua kubwa ya siku tano kuanza

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari kwa wananchi kuhusiana na mvua kubwa zinazotarajia kuanza kunyesha kuanzia jana kwa siku tano.

Kwa mujibu wa taarifa ya TMA, utabiri wa hali ya hewa unaonyesha mvua hizo zitanyesha ukanda wa Pwani ya Kaskazini katika mikoa ya Tanga, Visiwa vya Pemba na Unguja na mikoa ya Kanda ya Ziwa ya Kagera na Geita.

Taarifa hiyo ilitaja athari ambazo zilitarajiwa kujitokeza kuanzia jana na leo ni baadhi ya wananchi kuzungukwa na maji, ucheleshwaji wa usafiri, kusimama kwa muda kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Kwa kesho, Jumapili na Jumatatu kwa mujibu wa taarifa hiyo, hakuna tahadhari ambayo imetolewa.

Tangu kuanza kwa mvua hizi za vuli, baadhi ya mikoa imekumbwa na mafuriko na kusababisha vifo.

Hadi sasa vifo vilivyotokea vilivyosababishwa na mvua hizo ni zaidi ya 16, ambapo katika mkoa wa Morogoro kulikotokea vifo vya watu 11 kati yao watoto tisa wenye umri kati ya miaka 11 hadi 15.

Mkoa wa Tanga waliofariki ni watu sita wakiwamo watoto wanne na watu wazima wawili wamefariki dunia katika vijiji vya Bungu na Dindila wilayani Korogwe kutokana na kuangukiwa na nyumba kulikosababishwa na mvua kubwa.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Agnes Kijazi, alisema mvua hizo za msimu zitaendelea mpaka Desemba.

Licha ya kusababisha vifo, baadhi ya mikoa miundombinu mbalimbali ilipata changamoto ya kuharibika na baadhi ya nyumba kufunikwa na kusababisha wananchi kupata uharibifu wa mali zao zilizomo humo.

# Vikwazo 12 ufanyaji biashara vyaanikwa

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya serikali kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini, Ripoti ya Benki ya Dunia (WB) imetaja vikwazo 12 vya ufanyaji biashara nchini.

Katika ripoti hiyo ya mwaka 2019/20 imeonyesha kuwa Tanzania imeboresha baadhi ya mambo kiasi ya kuifanya kushika nafasi ya 141 kati ya 190 mwaka huu ikilinganishwa na nafasi ya 144 iliyoshika mwaka uliopita.

Maboresho hayo yameifanya Tanzania kushika nafasi ya nne katika nchi za Afrika Mashariki baada ya Rwanda, Kenya na Uganda.

Ripoti hiyo imeitaja Rwanda kushika nafasi ya 29 kati ya 190 ikiwa imeboresha kutoka nafasi ya 41 iliyoshika mwaka jana, huku Kenya ikishika nafasi ya 80 ikitoka nafasi ya 61 hadi mwaka 2018 ikilinganishwa na nafasi ya 80 mwaka 2017. Uganda imeshika nafasi ya 127 na Burundi 168, huku New Zealand ikiongoza.

Baada ya kutoa ripoti hiyo mwaka jana, Tanzania iliboresha baadhi ya mazingira ya ufanyaji biashara mojawapo ikiwa ni kuondoa urasimu, kubadilisha baadhi ya sheria, kupunguza baadhi ya kodi zilizokuwa kero kwa wafanyabiashara, pamoja na kupambana na rushwa.

Baadhi ya mabadiliko yaliyofanyika ni majukumu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Pia Tanzania imeanzisha kitabu cha maboresho kwa wafanyabiashara (Brueprint) ikiwa na dhumuni la kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara kwa wafanyabiashara.

Ripoti hiyo ilitaja vikwazo 12 ambavyo ilikuwa inaviangalia katika nchi husika ambavyo wafanyabiashara wanakumbana navyo.

Vikwazo hivyo ni mazingira ya kuanzisha biashara, kupata kibali

INAENDELEA UK. 8



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, SACP Gilles Muroto (kulia), akiwaonyesha waandishi wa habari jijini jana, wahamiaji haramu wanne kutoka nchi za Ethiopia na Somalia waliokamatwa juzi katika Kijiji cha Mtera, Wilaya ya Mpwapwa, mkoani humo juzi, wakisafirishwa kwa njia ya bodaboda wakitokea mkoani Arusha kuelekea mikoa ya kusini. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Wamiliki malori lazima kuwa na EFD

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetoa masharti kwa wamiliki wa malori yanayosafirisha mizigo nje ya nchi ikiwamo kila mmoja kuwa na mashine za risiti za kielektroniki (EFD) ili kupata leseni mpya ya usafirishaji.

Mwenyekiti wa Wamiliki wa Malori Wadogo na wa Kati (Tamstoa), Chuki Shaaban, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kutokana na mkutano waliofanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema katika kikao hicho walikaa na Kamishna wa Kodi za Ndani wa TRA ili kutafuta ufumbuzi juu ya ucheleweshaji mizigo inayokwenda nje ya nchi unaosababishwa na mashine ya EFD.

Shaaban alisema katika kikao hicho, walikubaliana na TRA kuwa ili kuondokana na ucheleweshaji huo, wasafirishaji mizigo nje ya nchi wanatakiwa kununua mashine za EFD.

"Lazima fedha ya usafirishaji ilipiwe kodi. Wasafirishaji wengi ilikuwa ikifika mwisho wa mwaka kwenye kukaguliwa kodi kunakuwa na changamoto, hivyo tumekubaliana magari yasikaguliwe mpaka watakapohakikisha kila mmoja ana mashine hizi," alisema.

Shaaban alisema moja ya vikwazo vya ucheleweshaji wa mizigo kilikuwa ukaguzi wa mashine ya EFD unaofanywa na TRA, hivyo wakakubaliana kwamba ili kukiondoa na madereva kutosumbuliwa, wamiliki wawe na mashine hizo.

"Tulipokaa na Kamishna wa Kodi za Ndani wa TRA, tulikubaliana moja kati ya viambatanisho vya kupata leseni kiwe risiti ya kununulia EFD ambayo ndiyo itamwezesha mmiliki kupewa leseni ya kusafirisha mzigo nje ya nchi," alisema.

Alisema mpaka kipindi cha mwisho cha kukata leseni, Tamstoa watakuwa na imani kwamba kila msafirishaji anakuwa na mashine ya EFD.

Baada ya kila mmoja kuwa na mashine hiyo, alisema ufuatiliaji wa matumizi yake utafanyika.

"Dereva anapokuwa na mashine ya EFD anaposimamishwa njiani, anampigia tajiri wake ina maana atakata hapo hapo risiti, hivyo mzigo hautachelewa na utafika kwa wakati. Tajiri (mmiliki) atakata na kumtumia dereva wake na mtu wa TRA ataingia kwenye mtandao kuhakikisha," alisema.

Endapo kila msafirishaji mizigo atakuwa na mashine ya EFD, alisema ma itasaidia serikali kukusanya kodi ipasavyo.

Alisema chama hicho kina zaidi ya wanachama 4,000 lakini kwa ujumla wadau wa usafirishaji wa malori nje ya nchi hawazidi 1,000.

Pia alisema katika kikao hicho walizungumzia kuhusu madalali wa mizigo ambao wako waaminifu na wasiowaaminifu.

"Tumebaini wanachama wetu wanashindwa kukitumia chama ipasavyo kutatua matatizo yao kwa sababu hawana anwani kamili ya chama. Hii imesababishwa na wamiliki wengi wa malori hutumia watu wa kati, hivyo tumeamua yeyote atakayekuja ili apate cheti lazima awe taarifa muhimu za mmiliki wa malori," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Madalali Wanaosafirisha Mizigo Nje ya Nchi, Rajabu Masasi, alisema chama chao kina madalali 100 na kilianza miaka mitatu iliyopita na mpaka sasa usajili haujakamilika.

## HABARI KITAIFA



Baadhi ya raia 87 wa Kichina waliokamatwa katika mgodi wa dhahabu wa Eagle Bland Investment uliopo katika eneo la Nyamahuna, kijiji cha Magenge, Kata ya Magenge, wilayani Geita, mkoani Geita wakifanya kazi bila kibali, wakiwa chini ya ulinzi jana. **PICHA: RENATUS MASUGULIKO**

# Wahamiaji haramu watumia mbinu mpya

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, limebaini mbinu mpya inayotumiwa na watu wanaosafirisha wahamiaji haramu.

Katika mbinu hiyo mpya, wasafirishaji hao wamekuwa wakitumia pikipiki ili kuwavusha wahamiaji kwenye mipaka badala ya malori na mabasi kama ilivyokuwa awali. Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kuwakamata wahamiaji wanne katika kijiji Mtera wilayani Mpwapwa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema kwa sasa wahamiaji hao wanasafirishwa kwa pikipiki kwa kuvushwa kwenye vizuizi na mipaka.

Muroto alisema polisi wamebaini mbinu hiyo mpya inayotumiwa na wasafirishaji hao kwa kuwatoa wahamiaji mikoa ya kaskazini ikiwamo Arusha na kuwapeleka mikoa ya kusini ili kwenda nchi wanazotaka ikiwamo Afrika Kusini.

Alisema juzi jeshi hilo liliwakamata wahamiaji hao walikuwa wakisafirishwa kwa pikipiki kutoka Arusha kwenda mikoa ya kusini.

Aliwataja wahamiaji hao kuwa ni Sellamu Yohanes (24) na Ashetu Tesfaye (20) wote raia wa Ethiopia na Mohamoud Mapaa (19) na Cuse Ciise (18) raia wa Somalia.

Muroto alisema jeshi hilo liliwakamata Watanzania wawili waliokuwa wakiendesha pikipiki kwa ajili ya kuwasafirisha wahamiaji hao.

Alimtaja mmoja wa Watanzania hao kuwa ni Jamali Babuu (26) mkazi wa Olasiti mkoani Arusha aliyekuwa akiendesha pikipiki yenye namba za usajili MC 942 AXK.

"Mwingine ni Wiston Makia (25) mkazi wa Mbauda mkoni Arusha aliyekuwa akiendesha pikipiki yenye namba za usajili MC 767 CEB," alisema.

Alibainisha kuwa watuhumiwa hao baada ya kukamatwa na polisi, walijaribu kuwarubuni askari kwa kutaka kuwahonga Sh. 500,000 na baada ya askari hao kukataa waliwasiliana na wenzao wa Arusha wakatumiwa Sh. 500,000.

Pamoja na kuongeza dau hilo, Muroto alisema askari hao walikataa na hatimaye kuwafikisha kituo cha polisi pamoja na fedha hizo.

# Rugemalira adaiwa kuugua mahabusu

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA James Rugemalira anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, jana alishindwa kufika mahakamani kusikiliza kesi yake kwa madai kuwa ni mgonjwa.

Hata hivyo, mshtakiwa mwenzake, Herbinder Seth, alifikishwa mahakamani kusikiliza kesi yao ikiwamo mashtaka ya kuisababisha serikali hasara ya dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa lakini amepata taarifa kwamba mshtakiwa Rugemalira ameshindwa kufika mahakamani kwa sababu ni mgonjwa.

Wankyo alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Shaidi alisema kesi hiyo itatajwa tena Novemba 7, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mapema mahakamani hapo, Rugemalira alidai kuwa amemwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) akiomba kuachiwa huru ili washirikiane kupata Sh. trilioni 37 mali ya serikali ya Tanzania.

Hata hivyo, wakati Rugemalira amemwandikia DPP kumwomba washirikiane kuzipata fedha za serikali, mwenzake Sethi amemwandikia mkurugenzi huyo kumwomba kukiri na kurejesha fedha kulingana na makubaliano watakayokuwa wameyafikia.

Wakili wa utetezi, Michael Ngalo, alidai kuwa mteja wake aliandika barua kwenda kwa DPP, lakini hawajapata majibu. Aliomba upande wa Jamhuri kusaidia majibu ya barua hiyo yapatikane.

Baada ya Wakili Ngalo kueleza hayo, Wakili Wankyo alidai kwamba ni kweli barua imepokewa na inafanyiwa kazi na kwamba majibu atapewa.

Rugemalira aliandika barua Oktoba 4, kwenda

INAENDELEA UK. 8


TANGAZO KWA UMMA

MATUMIZI MABAYA YA JINA LA

BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA KWA UDANGANYIFU

Tumepata taarifa za mawakala mbalimbali wanaojivika nafasi za uongo za kusaidia katika kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa nia ya kujipatia fedha. Udanganyifu huu mara nyingi hufanywa kwa kupitia barua-pepe, au njia nyingine za mawasiliano.

Benki ya Maendeleo ya Afrika inasikitishwa sana na udanganyifu huu, ambao ni ukiukwaji wa maadili ya taasisi, na itashirikiana na mamlaka zinazohusika kupambana na mtandao huo wa ulaghai.

**Sisi, Benki ya Maendeleo ya Afrika, tunathibitisha kwamba:**

- Hatudai wala kupokea malipo kutoka kwa watoa huduma, wagavi, wataalamu-washauri, wanaotafuta ajira, n.k., ili kuwapa mikataba ya kutoa huduma, ugavi wa bidhaa au malipo ili kutoa ajira.
- Tunatangaza waziwazi maombi yote ya manunuzi ya taasisi kwenye tovuti ya Benki, ambayo ni: **www.afdb.org/en/about-us/corporate-procurement**. Ikiwa ombi lolote la manunuzi halijatangazwa kwenye tovuti hiyo, ombi hilo halipo, ni ulaghai.
- Tunatangaza nafasi zote za ajira kwenye tovuti yetu: **www.afdb.org/jobseekers**. Kama nafasi ya ajira haijatangazwa kwenye tovuti hiyo, nafasi hiyo haipo, ni ulaghai.

Kwa hiyo, tunawashauri watu wote, pamoja na wafanya biashara wanaopenda kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuzingatia yafuatayo:

- Zingatia matangazo yanayohusu manunuzi, ambayo yanapatikana kwenye tovuti ya Benki tu, na si kwingineko.
- Kamwe usilipe au kutuma fedha kwa mtu yeyote ili kupata kazi, mkataba wa huduma au kufanya biashara yoyote na Benki.
- Toa taarifa za majaribio yote ya udanganyifu kwa mamlaka zinazohusika za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pia ifahamishe Benki kupitia anwani hii ya **barua-pepe: security@afdb.org.**

215468802



KUMBUKUMBU



215471902

**GRACE HEMED GUMBO**

**1940 – 2018**

Tarehe 25/10/2018 umemaliza mwaka mmoja tangu uitwe na Mwenyezi Mungu ingawa Mama yetu haupo nasi kimwili lakini kiroho tupo pamoja katika sala na maombi. Ulikuwa nguzo imara katika maisha yetu. Hekima na busara zako tutazikumbuka daima. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa maisha yako kwetu, hakika pengo ulilolacha halitazibika kamwe. Utakumbukwa daima na Mume wako Joseph Hemedi Gumbo. Watoto wako Joyce Gumbo, Charles Gumbo, Godfrey Gumbo, Peter Gumbo, Rodgers Gumbo, Elizabeth Gumbo, David Gumbo, Magreth Gumbo na Jestina Gumbo.

**Raha ya milele umpe ewe Bwana na mwanga wa milele umuangazie, apumzike kwa Amani. Amen!**

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 30.09.2019

**Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30-Septemba 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 30-Sep-19 | Robo Mwaka ya 30-Jun-19 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,054 | 4,415 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12,464 | 151,138 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 92,562 | 45,840 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,638 | 4,950 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 83,014 | 45,921 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 33,573 | 32,687 |
| 12 | Mali Nyingine | 5,483 | 4,900 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,318 | 1,389 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **237,106** | **291,240** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 118,784 | 189,108 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 16,582 | 16,660 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 45 | 10 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,411 | 1,851 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,825 | 681 |
| 27 | Dhima Nyingine | 851 | 1,087 |
| 28 | Madeni | 76,826 | 62,785 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **217,325** | **272,181** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **19,781** | **19,058** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (42,166) | (42,459) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,423 | 701 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | 293 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **19,781** | **19,058** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 847,525 | 859,254 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 232 | 1,163 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 592 | 1,446 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 8% | 7% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.68% | 3% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 25% | 17% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 14% | 11% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88% | 43% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -34% | 318% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -19% | 128% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-Septemba 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-19 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Jun-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 4,063 | 2,132 | 8,092 | 6,472 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,400) | (851) | (2,932) | (2,329) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,664** | **1,281** | **5,160** | **4,142** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (181) | - | (181) | (5) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,811** | **2,762** | **6,752** | **3,398** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 320 | 308 | 1,037 | 600 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,474 | 2,412 | 5,622 | 2,272 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 17 | 42 | 92 | 525 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(3,571)** | **(3,384)** | **(10,307)** | **(10,130)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,669) | (1,542) | (4,709) | (4,555) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (319) | (361) | (947) | (1,033) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,584) | (1,482) | (4,651) | (4,542) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **723** | **660** | **1,423** | **(2,595)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **723** | **660** | **1,423** | **(2,595)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **723** | **660** | **1,423** | **(2,595)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 117 | 114 | 117 | 105 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 115 | 105 | 226 | (413) |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 4 | 4 | 4 | 4 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.27% | 0.23% | 0.27% | -1.73% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3.72% | 3.46% | 3.72% | -13.34% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 60.79% | 69.14% | 60.79% | 102.64% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.60% | 1.03% | 1.60% | 3.08% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30-Septemba 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 30-Sep-19 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Jun-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-18 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **723** | **660** | **1,423** | **(2,595)** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 82 | 3 | 82 | 429 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (885) | (2,793) | (885) | 8,027 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (70,401) | 156,485 | (70,401) | 11,170 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (46,722) | (9,928) | (46,722) | (6,818) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (235) | 230 | (235) | 1,397 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (583) | 205 | (583) | 568 |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(118,022)** | **144,862** | **(117,322)** | **12,179** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (38) | (382) | (38) | (225) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(38)** | **(382)** | **(38)** | **(225)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 14,041 | 5,923 | 14,041 | 29,916 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **14,041** | **5,923** | **14,041** | **29,916** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(104,019)** | **150,402** | **(103,319)** | **41,870** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 239,664 | 89,262 | 89,262 | 81,294 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **135,645** | **239,664** | **(14,057)** | **123,164** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2019
(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2019** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (42,568) | - | 402 | - | 18,358 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,423 | - | - | - | 1,423 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(41,145)** | **-** | **402** | **-** | **19,781** |
| **Mwaka uliopita 2018** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (39,454) | - | 351 | - | 21,421 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | (3,048) | - | - | - | (3,048) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | (51) | - | - | - | (51) |
| Mengineyo | - | - | (16) | - | 51 | - | 35 |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(42,568)** | **-** | **402** | **-** | **18,358** |

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Usman Isiaka<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | ***Imesainiwa*** | ***25th September 2019*** |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | ***Imesainiwa*** | ***25th September 2019*** |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | ***Imesainiwa*** | ***25th September 2019*** |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | Imesainiwa | ***25th September 2019*** |
| 2 | Emeke Iweriebor<br>**Mkurugenzi** | Imesainiwa | ***25th September 2019*** |

215477702

UBA Africa's global bank

HABARI KITAIFA

# ACT-Wazalendo yakubaliwa kesi tafsiri ukomo wa urais

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imekubali ombi la Chama cha ACT-Wazalendo kujiunga kwenye kesi ya kikatiba iliyofunguliwa na Dezydelius Mgoya, maarufu kama Mkulima, kuhusu ukomo wa urais.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji Dk. Benhaj Masoud baada ya kusikiliza maombi ya ACT-Wazalendo kujiunga na kesi hiyo kwa sababu wana maslahi nayo.

Wakili wa ACT-Wazalendo, Jebra Kambole, alidai kuwa mteja wake ameomba kujiunga kwa sababu ni chama kilichosajiliwa na kimeshiriki katika uchaguzi.

Pia alidai kuwa chama hicho kina wanachama Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar kwa mujibu wa matakwa ya kisheria na katiba.

Mgoya alifungua kesi hiyo chini ya kifungu cha 4 cha sheria ya utekelezaji haki na wajibu, sura ya 3 ya mwaka 1994 chini ya Ibara ya 30(3) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Kwa mujibu wa hati ya madai ya kesi hiyo, Mgoya anahoji Ibara ya 40(20) ya Katiba ambayo imeweka ukomo wa mihula miwili tu ya miaka mitano mitano ya uongozi katika nafasi hiyo ya urais.

Hivyo anaiomba mahakama hiyo itoe tamko na tafsiri ya maana sahihi na athari za masharti ya ibara hiyo.

Pia anaiomba mahakama itoe tafsiri ya maana dhahiri ya masharti ya Ibara ya 42(2) ya Katiba kwa kuhusianisha na masharti ya Ibara za 13, 21 na 22 za Katiba hiyo.


Kadhalika, Mgoya anaiomba mahakama itoe tafsiri ya maana ya Ibara hiyo ya 40(2) kwa kuhusianisha na Ibara ya 39 ya Katiba.

# CCM yataka Zimbabwe kuondolewa vikwazo

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA Cha Mapinduzi(CCM), kimeyataka mataifa yote ambayo yameiwekea vikwazo Zimbabwe kuviondoa bila masharti yoyote.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara, Philip Mangula (pichanii), alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa katika mkutano wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), zililaani vikwazo ilivyowekewa nchi hiyo na kutaka iondolewe, lakini mpaka sasa jambo hilo halijatekelezwa.



Mangula alisema CCM kama sehemu ya vyama vya ukombozi katika Bara la Afrika, imetumia nafasi hiyo kupaza sauti kushinikiza mataifa yote ambayo yameiwekea vikwazo nchi hiyo kuhakikisha zinaviondoa.

Mangula alisema zipo athari mbalimbali ambazo Zimbabwe imezipata kutokana na kuwekewa vikwazo hivyo ikiwamo kushindwa kupiga hatua za maendeleo, kiuchumi, kuathirika katika namna mbalimbali kwa watoto, wanawake na vijana.

"Kwa kutambua jukumu letu katika kuimarisha umoja, mshikamano wa Waafrika na kuendeleza mapambano dhidi ya ukoloni mamboleo, kupiga vita ubeberu na ubaguzi wa aina yoyote pamoja na kuimarisha uhusiano mwema wa vyama vyote vya siasa vya nchi nyingine vyenye itikadi kama ya CCM, tunaamini kwamba vikwazo dhidi ya Zimbabwe ni mwendelezo wa fikra na matendo ya uovu," alisema Mangula.

Aliongeza: "Ni unyonyaji kwa Waafrika. Watu wa Zimbabwe wameonewa kiasi cha kutosha na sasa tunaazimia kuwa uonevu huo ufike mwisho, kuna watu wakati nchi hiyo inawekewa vikwazo walikuwa hawajazaliwa, lakini eti leo hii wanawekewa vikwazo, huku ni kuwaonea."

"Kwa tamko hili tunaweka msisitizo kupitia serikali ya Tanzania, SADC na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwamba ifike wakati Umoja wa Afrika uchukue nafasi yake na kusimamia haki za nchi wanachama, ambao kwa hila wanaendelea kuonewa kwa nguvu za kibeberu na ukoloni mamboleo."

Mangula alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali ya Zimbabwe katika kuimarisha demokrasia na uongozi bora na kujitegemea kiuchumi, lakini kutokana na vikwazo hivyo, imeshindwa kupiga hatua za maendeleo kwa kasi inayostahili.

Kwa upande wake Balozi wa Zimbabwe nchini, Anselem Sanyatwe, alikipongeza chama hicho kwa kuchukua hatua hiyo.

Alisema miongoni mwa sababu zilizochangia nchi hiyo kuwekewa vikwazo ni kutokana na uamuzi wake wa kuwanyang`anya wageni ardhi ambayo walikuwa wameipora na kuwarudishia wazawa.

"Tuliwekewa vikwazo kwa sababu ya mageuzi ya ukombozi baada ya kubadili sera ya umiliki wa ardhi kwa asilimia 75 iliyokuwa ikimilikiwa na wageni, jambo hilo halikuwafurahisha na kuamua kutushtaki EU (Muungano wa Ulaya) ambayo iliamua kutuwekea vikwazo. Lakini tayari ni miaka 19 sasa tangu tuwekewe vikwazo hivyo, hii siyo sawa kabisa kwa sababu wanaoathirika ni vizazi vipya, wale waliosababisha haya wengine tayari wameshakufa," alisema Balozi Sanyatwe.


## UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED
## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES

| S/N | ITEM/TRANSACTION | | |
|---|---|---|---|
| SECTION A | SAVINGS ACCOUNTS | RETAIL | CORPORATE |
| 1 | FREEDOM SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 5,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 2 | GENERAL SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| 3 | EMPLOYEE SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS15,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 USD 10 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Adhoc statement request | TZS 1,000/ PAGE | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 4 | SAVINGS ACCOUNT INDIVIDUALS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 5 | SAVINGS ACCOUNT SALARY | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 6 | SAVINGS ACCOUNT DOMICILARY | | |
| | Required minimum opening balance | USD10 | |
| | Minimum operating balance | USD 5 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1% per Transaction | |
| | Closing account | USD 5 | |
| 7 | U-CARE CHILDREN SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| SECTION B | CURRENT ACCOUNTS | | |
| 1 | INDIVIDUAL CURRENT ACCOUNT | | BUSINESS CURRENT ACCOUNT |
| | Required minimum opening balance | TZS 30,000 | TZS 100,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 10,000 | TZS 100,000 |
| | Monthly maintenence fee | TZS 10,000 | TZS 12,000 |
| | Cash withdrawal at counter | 1 PER MILLE | TZS A/C 1 PER MILLE |
| | Closing account | TZS 10,000 | TZS 10,000 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 10% | TZS A/C PLR + 10% |
| 2 | DIPLOMAT ACCOUNTS | | |
| | Required minimum opening balance | USD 200 | N/A |
| | Minimum operating balance | USD 100 | N/A |
| | Monthly maintenence fee | NIL | N/A |
| | Cash withdrawal at counter | NIL | N/A |
| | Closing account | NIL | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | NIL | N/A |
| | Outward fund transfers(TTs) | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 | N/A |
| | Inward fund transfers(TTs Incoming) | NIL | N/A |
| | FOREX exchange | Favourable rates will be applied | N/A |
| 3 | DOMICILIARY CURRENT ACCOUNT | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Minimum operating balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Monthly maintenence fee | USD 12 or its equivalent | USD 15 or its equivalent |
| | Minimum search fees | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 |
| | Cash withdrawal | 1% per Transaction | 1% per Transaction |
| | Cheque book - 25 LEAF | USD 10 or its equivalent | N/A |
| | Closing account | USD 10 | USD 10 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 2% | PLR + 2% |
| | Transfer From TZS to DOMICILIARY/ DOMICILIARYto TZS | NIL | NIL |
| SECTION C | DEPOSIT ACCOUNTS | | |
| 1 | Call Accounts | | Call Accounts |
| | Minimum opening balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Monthly Average balance requirement | Negotiable | Negotiable |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| 2 | Term Deposits | | Term Deposits |
| | Minimum deposit - local currency | TZS 500,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum deposit - USD | USD 1,000 | USD 10,000 or equivalent |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| SECTION D | ELECTRONIC BANKING | | |
| 1 | E-Banking | | E-Banking |
| | Internet banking monthly subscription | TZS 2,000 Per Month. | TZS 10,000 per Month |
| | Internet banking ( Re issue pin) | TZS 5000 | TZS 5000 |
| | U - Direct (Reversal of transaction) | TZS 4000 | TZS 4000 |
| | E-statement (self downloaded) | FREE | FREE |
| | POS purchase (Local) | FREE | N/A |
| | POS purchase (International) | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| | ATM reversal | TZS 1,000 per transaction | N/A |
| | Fund transfer/ company load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Card Load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Manual pin change | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per transaction |
| | U-MOBILE(mobile banking-Bank to wallet) | TZS 1,000 (0 - 200,000/=) and TZS 2,000 (200,001 - 400,000/=) | N/A |
| | Card to card transfer | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per tr |
| | Africash | TZS 6000 + 1.5% of the amount sent/USD 4.45 + 1.5% | N/A |
| 2 | Visa Debit Card | | N/A |
| | Issuance fees | TZS 10,000 | |
| | Re-issuance fee | TZS 10,000 | |
| 3 | Visa Perapid Cards | | N/A |
| | Issuance fees for instant card | TZS 12,000 | |
| | Issuance fees for personalized card | TZS 16,000 | |
| | Re-issuance fees | TZS 12,000 | |
| | Online Passcode reset fee | TZS 1,500 | |
| | ATM Pin reset fee | TZS 1,500 | |
| | Loading fee | TZS 1,000 | |
| | Online shopping fee - Local transactions | FREE | N/A |
| | Online shopping fee/Web - Int. transactions | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| 4 | ATM Withdrawals | | N/A |
| | At UBA ATMs (On us) | TZS 500 | |
| | ATM Balance inquiry(Local) | TZS 200 | |
| | ATM Balance inquiry(international) | TZS 1000 | |
| | To other banks ATM (On others/OFF US)Local | TZS 2,500 | |
| | international ATM withdraw | TZS 6000 | |
| SECTION E | ASSET BANKING | | |
| 1 | LOANS | | |
| | Processing fee | negotiable | 2% |
| | Insurance for personal loans | N/A | 1.50% |
| | Legal fees | 0.5% minimum of TZS 300,000 | 0.5% minimum of TZS 300,000 |
| 2 | TEMPORARY OVERDAFT (TODs) | | |
| | Processing fee | 2% | 2% |
| SECTION F | TRADE FINANCE | | |
| 1 | Guarantees | | Guarantees |
| | Facility Commission | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qrt. | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qtr. |
| | Arrangement fees | 2% | 2% |
| | Cash Covered | 0.5% per qtr Min 250 per qtr | 0.5% per qtr Min 250 per qtr |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| | Extension to next quarter | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) |
| | Amount increase | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) |
| 2 | Letters of Credit - Imports | | Letters of Credit - Imports |
| | Issuance commision | 0.5% per quarter. Min USD 150. | 0.5% per quarter. Min USD 150. |
| | Handling Fees | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| 3 | Letters of Credit - Exports | | Letters of Credit - Exports |
| | LC Advising Commission | USD 200 flat | USD 200 flat |
| | Amendment advising commision | USD 100 Flat | USD 100 Flat |
| | Correspondences Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Documents handling and examination fee | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 |
| | Courier charge | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | LC confirmation charges | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) |
| 4 | Letters of Credit Refinancing | | Letters of Credit Refinancing |
| | Interest on refinance | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on refinance | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 5 | Discounting on LC/Invoice/Cheque | | |
| | Interest on discounting | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on discounting | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 6 | Bills Discounting (Bills of exchange including cheques) | | |
| | Interest on discounting | PLR +3%-local; International Lobor+8% | PLR +3%-local; International Lobor+8% |
| 7 | Documentary Collection - Export | | |
| | Handling charge | 0.25% of the invoice min USD 100 flat | 0.25% of the invoice min USD 100 flat |
| | Courier charge | USD 100 | USD 100 |
| | Corespondence commission | USD 50 Per tracer | USD 50 Per tracer |
| 8 | Documentary Collection - Import | | |
| | Handling Commission | 0.25%. Min USD 100 | 0.25%. Min USD 100 |
| | correspondence Swift charge | USD 50 | USD 50 |
| 9 | Outward Bills for Collection (clean collections & TCs) | | |
| | Handling Commision | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent |
| | Dhl charges | usd 75 flat | usd 75 flat |
| | Returned foreign cheques | claimed charges + locally un re-covered charges | claimed charges + locally un re-covered charges |
| 10 | Inward Bills for Collection | | |
| | Handling Commission | USD 50 flat per collection | USD 50 flat per collection |
| | Swift charged | USD 40 flat per collection | USD 40 flat per collection |
| 11 | Local Currency Transactions | | Local Currency Transactions |
| | Outward remittances (TISS) | TZS10,000 PER TRANSACTION | TZS10,000 PER TRANSACTION |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT |
| | Inward Swift Transfers (TISS) | NIL | NIL |
| 12 | Foreign Currency Transactions | | Foreign Currency Transactions |
| | Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 |
| | Telegraphic Overseas Charges/ OURS | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | Inward Swift Transfers | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | International Money Order (IMO) | USD 30 per IMO | USD 30 per IMO |
| | Foreign cheques for collection | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; |
| SECTION G | OTHERS | | |
| 1 | Statements | | Statements |
| | Monthly | FREE | FREE |
| | Adhoc requests | TZS 1,000/ PAGE | TZS 1,000/ PAGE |
| 2 | Cheque Books Issuing | | Cheque Books Issuing |
| | - 25 Leaf | TZS 15,000; USD 10 | N/A |
| | - 50 Leaf | TZS 30,000; USD 20 | N/A |
| | - 100 Leaf | TZS 45,000; USD 30 | TZS 45,000; USD 30 |
| | Counter cheque request | TZS 20,000; USD 10 | TZS 20,000; USD 10 |
| | Cheque Stop payment instructions | leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; | Leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; |
| | Issuance of Manager's cheque | TZS 25,000; USD 20 per item | TZS 25,000; USD 20 per item |
| | Managers cheque cancellation charges | FREE | FREE |
| 3 | Standing order | | Standing order |
| | Standing order set-up | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Standing order maintanance | NIL | NIL |
| | Standing order/Foreign Bank (TT charge) | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 |
| | Amend / Stop standing Order | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Unpaid standing order | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent |
| 4 | Insufficient funds/effects not cleared | | Insufficient funds/effects not cleared |
| | Effects not cleared | **ITEM REMOVED** | **ITEM REMOVED** |
| | Insufficient Funds (Refer to drawer) | TZS 50,000; USD 50 | TZS 50,000; USD 50 |
| 5 | Other services/charges | | |
| | Retriving old documents (2-6 months) | TZS 10,000; USD 10 | TZS 10,000; USD 10 |
| | Retriving documents (6 months and above) | TZS 15,000; USD 15 | TZS 5,000; USD 15 |
| | Confirmation/Audit/ Certificate of balance | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent |
| | Status enquiry / Reference Letters | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent per customer request | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent |
| | Manual processing of salaries | TZS 1,000; USD1 or its equivalent | TZS 1,000; USD1 or its equivalent |
| | Closure of Account | TZS10,000 | TZS10,000 |
| | Dormant Account Reactivation | FREE | FREE |
| | Cash handling fee-COINS ONLY | 9% of the Deposit | 9% of the Deposit |
| 6 | Soiled notes | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| 7 | Coins | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| | | | |
| | **approved by:** | | |
| | **Signature:** | | **Signature:** |
| | | | |
| | Flavia Kiyanga | | Chomete Hussein |
| | **Chief Operating Officer** | | **Country Chief Finance Officer** |
| | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** | | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** |
| | **Disclaimer: All fees are VAT exclusive.** | | |

UBA
Africa's global bank

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tumeona hakuna kama wewe UN

**UMOJA** wa Mataifa (UN) sasa umetimiza miaka 74. Hongera rafiki kipenzi UN, umekuwa chanzo cha maendeleo, ushirikiano, umoja na ulinzi wa amani na haki za binadamu duniani.

Tumeona mambo mengi na mafanikio duniani yakipatikana kupitia mkono wa Umoja wa Mataifa. Kwa miaka mingi umekuwa rafiki wa Afrika, ukisaidia kuleta mipango na mikakati mbalimbali pamoja na rasilimali za kuondoa umaskini.

Tunashuhudia mashirika yake kama lile la watoto -UNICEF likihimiza, kusimamia na kusaidia kwa hali na mali maisha bora na afya endelevu ya watoto wetu kuanzia chanjo na hata dawa muhimu.

Si hivyo, tu jumuiko hilo, limewezesha kupambana na vifo vya wajawazito, wazazi na watoto kupitia miradi mbalimbali ya afya iliyokuwa inaainishwa kwenye programu ikiwamo ya maendeleo ya milenia.

Aidha, UN kupitia Shirika la Afya WHO imekuwa mstari wa mbele kupambana na maradhi yanayotishia dunia na hasa Afrika ili kuendeleza ustawi wa watu, afya na maisha bora.

Kwa sasa hakuna anayepingana na kazi kubwa inayofanywa na WHO kupambana na kudhibiti kitisho cha ebola Afrika na kuzuia maangamizi makubwa ambayo yangetokea iwapo ugonjwa huo usingedhibitiwa kwa jitihada hizo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, anapozungumza katika maadhimisho ya kuzaliwa UN anasema Tanzania imejipanga kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) ya UN kwa kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Anapozungumza huko Dodoma kwenye kusherehekea siku ya kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa inayoongozwa na kauli mbiu 'Wanawake na Wasichana katika mstari wa mbele kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG)'.

Anawahakikishia wadau na UN kuwa serikali imewekeza kwenye miradi mikubwa kama vile ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), barabara, bandari, viwanja vya ndege na bwawa la kufua umeme Rufiji ili kuwa na uwezo wa kiuchumi wa kutoa huduma kwa wananchi wake. Anakumbusha kuwa uwekezaji mkubwa kama huo hauwezi kutenganishwa na miradi ya maendeleo ya kijamii kama kutoa elimu bure, huduma za afya, maji safi na salama pamoja na kuimarisha uchumi.

Kwa vile jambo kubwa la UN kwenye maadhimisho hayo ni usawa wa kijinsia na ushiriki wa wanawake kwenye maendeleo endelevu, Tanzania haina budi kulitekeleza kwa vitendo.

Waziri wa Mambo ya Nje, anapozungumzia suala la ukatili wa kijinsia anasema ni lazima kuukomesha ukatili huo na taifa linatoa kipaumbele.

Anasema kuna mkakati wa kuleta usawa wa kijinsia ambao baadhi ya mambo yanayofanyika hata sisi tunayashuhudia.

Mojawapo ni Rais John Magufuli, kusimamia kwa dhati na kuwataka viongozi wa serikali kuanzia wabunge, polisi, wanasheria, wakuu wa mikoa na wilaya kumaliza suala la mimba za utotoni na ndoa za mabinti.

Aidha, pamoja na kutaka suala hilo kutokomezwa serikali inasimamia utoaji wa mikopo ya riba nafuu kwa vijana, kinamama na walemavu ili wawekeze na kuanzisha miradi ya maendeleo.

Tunaomba hatua zichukuliwe zaidi kuimarisha ustawi wa wanawake na mabinti lengo likiwa ni kutimiza azma ya UN kupitia kauli mbiu 'Wanawake na Wasichana katika mstari wa mbele kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG)'.

Tunaamini kukomeshwa ukatili dhidi ya wanyonge hawa, kuboresha huduma za uzazi salama, kupewa nyenzo na mitaji ya uwekezaji, kupata elimu na kushirikishwa kwenye nafasi za uongozi za kisiasa, kijamii, kiuchumi wanawake wa Tanzania watakuwa na nafasi nzuri ya maendeleo endelevu.

Tunapoungana na UN kusherehekea kutimiza miaka 74 tunaona kuwa kipaumbele chetu kiwe maendeleo endelevu kwa wote ili tuwe na Tanzania yenye amani na furaha kwa raia wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






# Muungwana Lazima Nilonge

## Habari njema ya lami tangu Uhuru na matumizi mapya

Na Sabato Kasika

**KINACHOENDELEA** kwa sasa Musoma Vijijini mkoani Mara, ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, ili kurahisisha usafiri wa magari ya abiria na mengine ya biashara.

Mbali na hilo, barabara hiyo pia itakapokamilika, inatarajiwa kuwasaidia jumuiya ya eneo hilo kuwahi kwenye huduma mbalimbali. Wagonjwa nao wanarahisishiwa safari ya kwenda hospitali ya wilaya inayojengwa kwenye kitongoji cha Kwikonero katika kijiji cha Suguti.

Ni barabara maarufu kama 'Barabara ya Musoma hadi Busekera' na inajengwa kwa kiwango cha lami, kuanzia katika kijiji cha Kusenyi hadi Suguti, ujenzi wa hospitali ya wilaya unaendelea. Kwa kipindi kifupi cha siku zilizopita, nilizokuwa Musoma Vijijini, nilishuhudia ujenzi wa barabara hiyo ukiendelea kwa kasi. Udongo unahamishwa na kuwekwa mwingine.

Magari yalikuwa yanasomba udongo na 'makatapila' yakifanya kazi ya kusawazisha mabonde na miinuko kwenye barabara hiyo, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kuweka lami.

Kwa ujumla, maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami yanakwenda kwa kasi, bila ya kuathiri shughuli za usafiri kwenye barabara hiyo kuu kutoka Musoma hadi Busekera.

Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, anatoa ufafanuzi wa ujenzi huo, kwamba ni umbali wa kilomita tano za mwanzo zitakazoishia eneo ambalo hospitali ya wilaya inajengwa.

"Zitajengwa kilomita tano kwanza, serikali itakamilisha ujenzi wa kilometa zote 92... Musoma, Makojo hadi Busekera baadaye," Profesa Muhongo.

Barabara hiyo inapojengwa kwa kiwango cha lami, itasaidia kurahisisha usafiri kwa wakazi wa Musoma Vijijini na hata usafirishaji wa mazao mbalimbali, yakiwamo ya biashara kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Jambo la msingi ni kwamba,wahusika wanapaswa kuhakikisha ujenzi huo unakamilika, ili kurahisishia wananchi usafiri wa kutoka eneo moja, kwenda lingine, ndani yake kuna manufaa ya kurahisishwa kwenda kupata huduma ya afya.

Katika hatua hiyo ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, mbunge anaeleza imani yake kwa kaulimbiu yake inaendelea kutumika jimboni anakotumikia "Maendeleo kwa Vitendo".

Anafafanua kwamba, barabara hiyo ikikamilika itahudumia vijiji 68 vya kata 21 ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini, ikiwa mara ya kwanza eneo hilo kuwa na barabara ya lami tangu nchi ilipopata uhuru mwaka 1961.

Kuwapo ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, kunawapa matumani mapya baadhi ya wakazi wa vijiji vya Kusenyi na Suguti wanaoamini kwamba hivi sasa wataepuka adha ya kukwama barabarani, pindi mvua zitakaponyesha.

Sadick Chiguma, mkazi wa kijiji cha Suguti anayesema eneo hilo lina udongo mwekundu unaonata, ambao wakati wa mvua umekuwa ukisababisha magari kukwama.

"Lakini wakati huu ambao ujenzi umeanza, mafundi wamesomba changarawe na kutuwekea barabarani, ili magari yasikwame na wanaendelea na ujenzi kama kawaida wakati huu wa mvua," anasema Chiguma.

Anasema, hiyo ni dalili tosha kuwa lami ikishawekwa, changamoto za kukwama wakati wa mvua zitakuwa zimeisha, hivyo kuwafanya wasafiri bila tatizo hata wakati wa masika. "Miaka yote tumekuwa tukipata shida kutoka Kusenye hadi Suguti wakati wa mvua, lakini ninaamini tatizo hilo limepatiwa ufumbuzi baada ya serikali kuanza kutowekea lami," anasema Amani Nackson kutoka Kusenyi.

Anasema, ingawa lami ni kwa ajili ya kilometa tano za kwanza, bado wanaifurahia, kwa vile ni mara ya kwanza eneo hilo kupata lami na ana uhakika kuna mambo mengi ya maendeleo yatakayopelekwa Musoma Vijijini.

"Tunajengewa hospitali ya wilaya na kuwekewa lami kwenye barabara kuu ya Musoma hadi Busekera...hii ni habari njema kwetu na tunaipongeza serikali kwa uamuzi huu muhimu kwa ajili yetu," anasema. Kimsingi, wanachosema ni sahihi, kwa sababu kuwapo lami ni moja ya maendeleo, kwa kuwa inaweza kusaidia kuwarahisishia usafiri na pia huduma nyingine za msingi zikiwamo kusafiri na kuwahi huduma za afya.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, akizungumza katika maonyesho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria, yanayofanyika mkoani humo, juzi, ambayo kilele chake ni leo.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kabudi afichua mikakati ya kufikia maendeleo endelevu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema Tanzania imejipanga kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) kwa kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Kauli hiyo aliitoa jana katika maadhimisho ya miaka 74 ya kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa (UN) iliyofanyika jijini hapa yenye kauli mbiu 'Wanawake na Wasichana katika mstari wa mbele kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG)'.

Alisema serikali imewekeza kwenye miradi mikubwa kama vile ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), barabara, bandari, viwanja vya ndege na bwawa la kufua umeme Rufiji ili kuwa na uwezo wa kiuchumi wa kutoa huduma kwa wananchi wake.

"Hatuwezi kutenganisha miradi hii ya kimkakati na maendeleo ya kijamii, ili tuweze kutoa elimu bure, huduma za afya, huduma za maji na zingine lazima tuimarishe uchumi wetu, lazima tuwe na miundombinu na nishati," alisema.

Prof. Kabudi alisema si mara ya kwanza Tanzania kutoa elimu bure ambapo mwaka 1960 na 1970, lakini baada ya hapo ilishindwa.

"Kwanini sasa baada ya hapo ilishindwa kwa sababu elimu hiyo ilitegemea misaada kutoka nje ya nchi, tulitoa huduma za afya bure, lakini ilitegemea misaada kutoka nje, tulijenga miradi ya maji, lakini ilitegemea misaada kutoka nje, sasa tunataka kujitegemea," alisema.

Alibainisha kuwa ili waweze kutoa huduma hizo, lazima wawekeze kwenye uchumi kwa kujenga miradi mikubwa.

"Reli hii inayotumika sasa imejengwa wakati wa ukoloni wa Wajerumani, imetusaidia kwa miaka zaidi ya 100 sasa ni wakati wa kujenga ya kwetu, ingawa tutaendelea kuwa na hii ya Wajerumani, lakini lengo ni kuwa na uchumi imara ili kuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi," alisema.

Prof. Kabudi alisema hatua hiyo ya kuimarisha uchumi itawezesha kugharamia huduma za kijamii na ni wakati wa kuwa na uchumi wa kujitegemea.

"Aidha, alisema hakuna sababu ya kubabaishwa na wale wanaofikiri wanaweza kusimama wenyewe kwa kuwa wana nguvu bila kuwa na ushirikiano na UN.

Aliwataka watu kuwapuuza wanaodhani hakuna mabadiliko ya tabianchi, wakati uharibifu wa mazingira unaendelea kuathiri.

"Hii imeongeza upatikanaji wa mitaji kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na kupeleka jumla ya Sh. bilioni 8.04 na kutolewa kwa vikundi vya wanawake 3,835 kwa mwaka 2018/19," alisema.

Alihimiza halmashauri kuendelea kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kiuchumi.

Kuhusu ukatili wa kijinsia, Prof. Kabudi alisema suala la kukomesha ukatili wa kijinsia limepewa kipaumbele na serikali ya awamu ya tano kwa kuwa na mpango maalum wa kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto.

Alisema Dunia inakabiliwa na changamoto mbalimbali za maendeleo na matishio ya kiusalama kama vile ugaidi, vita, migogoro mbalimbali na mabadiliko ya tabia nchi.

Naye Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), Jacqueline Mahon, alisema UN itaendelea kushirikiana kwa karibu na Tanzania na washirika wengine ili kuongeza kasi ya lengo namba tano la kuleta usawa wa jinsia na kuwezesha wanawake na wasichana.

Pia alisema idadi ya kesi za ukatili wa kijinsia zilizotolewa taarifa katika wilaya zinazosaidiwa na UN inazidi kuongezeka kadiri wanawake na wasichana wanavyopata uelewa zaidi ambapo kesi 20,000 zilifunguliwa kwa mwaka 2017/18.

"Hadi kufikia mwaka 2018, zaidi ya wasichana 135,000 katika zaidi ya shule 1,500 kote Tanzania wamewezeshwa kushiriki katika kufanya uamuzi uliokuwa na matokeo chanya katika kujifunza kwao, afya zao na kinga yao," alisema.

# Taasisi ya Dk. Ntuyabaliwe 'yanoa' wanafunzi ujasiriamali

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Dk. Ntuyabaliwe, imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kinondoni jijini Dar es Salaam ili kuwaandaa watakapomaliza masomo badala ya kusubiri kuajiriwa wajiajiri wenyewe.

Ofisa Elimu wa Kata ya Mwananyamala, Joshua Biswalo, akifunga mafunzo hayo yaliyofanyika shuleni hapo, alisema wazazi na walezi wanatakiwa kuunga mkono jambo hilo ili kuendeleza elimu ya ujasiriamali waliopata watoto hao. Mafunzo hayo yajulikanayo kama 'Future Centillionear', yametolewa kwa wanafunzi 11 wa darasa la sita kwa wiki sita na taasisi hiyo ambayo Mkurugenzi wake ni Jacqueline Mengi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, ofisa huyo wa elimu aliwataka wazazi kutowazuia watoto wao wawapo nyumbani kuendeleza elimu ya ujasiriamali waliyoipata.

"Tumeshuhudia watoto hawa kupitia mafunzo haya ya muda mfupi, wametengeneza kadi, vibubu vya kuhifadhia fedha na mifuko ya kuwekea bidhaa mbalimbali, vitu hivi walivyotumia vinapatikana kwenye maeneo yetu. "Wawapo nyumbani kwa sababu vitu hivi ni vile ambavyo vimeshatumika, wanaweza kuviokota na kutengeneza bidhaa nyingine, msiwakataze."

Biswalo aliwataka wanafunzi waliopata mafunzo hayo, wawafundishe na wenzao ili elimu hiyo waipate wanafunzi wote.

Jacqueline alisema Taasisi ya Dk. Ntuyabaliwe wakati ikianzishwa, ililenga kuhimiza watoto kupenda kujisomea vitabu, hivyo wameshaboresha maktaba kwenye baadhi ya shule jijini Dar es Salaam, Morogoro na wiki ijayo watakwenda Dodoma.

Pia alisema taasisi hiyo ilianzisha shindano la 'Andika Challenge' ambalo lilihusisha shule mbalimbali jijini Dar es Salaam.

"Tunataka watoto waliopo shule waanze kujifunza ujasiriamali mapema, tumeanza na Shule ya Msingi Kinondoni kwa kutoa mafunzo kwa wanafunzi 11 wajifunze ujasiriamali, umri wao ni mwafaka wa kujifunza vitu ili baadaye wakimaliza shule wanaweza kuchagua kuajiriwa ama kujiajiri," alisema. Mwanafunzi wa darasa la sita shuleni hapo, Jenifa John, akisoma risala kwa niaba ya wenzake, aliishukuru taasisi hiyo kwa kuwakumbuka na kuwapa mafunzo hayo muhimu.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Adelina Kessy, alisema uwapo wa maktaba, shindano la Ubongo Challenge na sasa mafunzo ya ujasiriamali, yamewezesha wanafunzi kupanua uelewa zaidi na wanapofundishwa darasani wanajibu maswali ipasavyo.

Mwenyekiti wa wazazi wa shule hiyo, Swed Twaibu, alisema licha ya idadi kubwa ya wanafunzi shuleni hapo, katika matokeo ya mitihani ya darasa la saba iliyotangazwa hivi karibuni, shule hiyo imefanya vizuri na kupanda daraja.




# Rugemalira adaiwa kuugua mahabusu

INATOKA UK. 3

kwa DPP na kupokewa siku iliyofuata huu akiomba aachiwe huru ili kushirikiana na serikali kupata Sh. Trilioni 37 kutoka Benki ya Standard Cherterd na washirika wake.

Katika kesi ya msingi, Sethi na Rugemarila wanakabiliwa na mashitaka 12 ya uhujumu uchumi ikiwamo kula njama, kujihusisha na mtandao wa uhalifu, kughushi nyaraka, kutoa nyaraka za kughushi, kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu, kutakatisha fedha na kuisababisha Serikali hasara ya dola za Marekani 22, 198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa Oktoba 18, 2011 na Machi 19 , 2014 jijini Dar es Salaam, walikula njama katika nchi za Afrika Kusini, Kenya na India ili kutenda kosa.

Aidha, inadaiwa katika mashtaka ya kujipatia fedha kwamba kati ya Novemba 28 na 29, 2011 na Januari 23,2014 katika Makao Makuu ya Benki ya Stanbic Kinondoni na Benki ya Mkombozi tawi la Mtakatifu Joseph, kwa ulaghai walijipatia kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Pia washtakiwa wote wanadaiwa kuisababishia serikali hasara kwa kutenda makosa hayo Novemba 29, 2013 katika Benki ya Stanbic, makao makuu Kinondoni, kwa vitendo vyao waliisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 22, 198, 544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Kati ya Novemba 29,2013 na Januari 23, 2014 maeneo tofauti Dar es Salaam kwa pamoja walitenda kosa la kutakatisha fedha kwa kuchukua fedha kutoka BoT ambazo ni dola za Marekani milioni 22.1 na Sh. bilioni 309.4 wakati wakijua fedha hizo ni zao la kujihusisha na genge la uhalifu.

# OCS Oysterbay aitwa mahakamani

**Na Hellen Mwango**

MKUU wa Kituo cha Polisi Oysterbay na Kijitonyama, jijini Dar es Salaam ametakiwa kufika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, kuieleza sababu za kukaa na mshtakiwa Elizabeth Balali (54), aliyeandikiwa hati ya kupelekwa mahabusu ya Segerea Oktoba 10, mwaka hii.

Elizabeth ni mke wa marehemu na msimamizi wa mirathi, alifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza akikabiliwa na kesi ya Ujumumu Uchumi ikiwamo ulaghai, kujipatia Sh. milioni 25 na kutakatisha fedha. Amri hiyo ilitolewa jana alasiri na Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kevini Mhina, baada ya mshtakiwa huyo kukaa Kituo cha Polisi Kijitonyama badala ya kupelekwa Segerea kama hati ya mahakama hiyo ilivyoelekeza.

Mapema Oktoba 10, mwaka huu Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, alimsomea mshtakiwa huyo mashtaka yake kwamba kati ya Oktoba 19 na Desemba 21, 2017 Dar es Salaam, alijipatia kiasi cha Sh. milioni 25 kutoka kwa Dk. Roderick Kisenge kwa ulaghai.

Mshtakiwa anadaiwa kujifanya anamuuzia Dk. Kisenge eneo la mita za mraba 900 ambalo halijapimwa lililopo eneo la Boko Dovya, Kinondoni wakati akijua eneo hilo si lake.

Wankyo alidai katika kipindi hicho mshtakiwa huyo alipokea kiasi hicho cha fedha kutoka kwa Dk. Kisenge, kupitia akaunti yake iliyopo Katika Benki ya CRDB wakati akijua fedha hizo ni zao la kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Baada ya kusomewa mashtaka, Elizabeth hakuruhusiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza makosa ya Uhujumu Uchumi.

Hakimu Mhina alimfahamisha mshtakiwa huyo kuwa licha mahakama kutokuwa na uwezo wa kuisikiliza kesi hiyo, pia shtaka la utakatishaji wa fedha halina dhamana.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi haujakamilika. Kesi iliahirishwa hadi siku jana wakati mshatakiwa alitakiwa kupelekwa rumande Segerea, lakini alipelekwa kituo cha polisi.



Waziri wa Sheria wa Palestina, Mohamad Shalaldeh, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akiishukuru Serikali ya Tanzania, kwa kupaza sauti ili nchi ya Palestina ipate uhuru wake. Kulia ni Balozi wa Palestina hapa nchini, Hamdi Abuali. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Vikwazo 12 ufanyaji biashara vyaanikwa

INATOKA UK. 2

cha ujenzi, upatikanaji wa umeme, usajili wa bidhaa, kuwalinda wawekezaji, makato katika kodi, uingizaji wa bidhaa mipakani, uingiaji wa mikataba, kuajiri wafanyakazi, pamoja na mikataba kati ya wawekezaji na serikali.

Ripoti hiyo ilieleza kuwa kipengele cha uanzishaji wa biashara walikuwa wakiangalia utaratibu, muda na gharama za uanzishaji wa biashara katika nchi husika.

Kwenye kigezo cha kibali, waliangalia utaratibu, muda, gharama za kumaliza ujenzi wa maghala ya kuhifadhi bidhaa, kwenye kigezo cha umeme waliangalia upatikanaji wa umeme wa kutosha kuwezesha viwanda kufanya kazi kwa wakati wote.

Ripoti hiyo ilieleza kuwa kwenye usajili wa bidhaa, waliangalia utaratibu wa kusajili biashara, muda na gharama za kukamilisha taratibu zote hadi mfanyabiashara anaanza kufanya biashara.

Kuwalinda wawekezaji, ripoti hiyo ilieleza kuwa waliangalia namna serikali husika inavyolinda haki za wawekezaji, kwenye ulipaji wa kodi na muda wanaopewa wafanyabiashara wa ulipaji kodi.

Kwenye kipengele za uingizaji bidhaa mipakani, ripoti hiyo ilieleza kuwa iliangalia muda na gharama za kuingiza bidhaa kutoka ndani na nje ya nchi.

"Togo ni miongoni mwa nchi zilizoboresha mazingira ya kufanya biashara kwa mwaka wa pili sasa, wameboresha ada ya kibali cha ujenzi, pamoja na usajili wa bidhaa. Nigeria ipo katika marekebisho ya baadhi ya viashiria," ilieleza ripoti hiyo.

Aidha, ilieleza kuwa baadhi ya nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kama Afrika Kusini, Liberia, Burundi, Afrika ya Kati na Namibia zimeendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara ikiwamo upatikanaji wa umeme wa kutosha, mfano wafanyabiashara wanalipa zaidi ya asilimia 3,100 ya wanachoingiza kwa siku ili waunganishwe katika gridi.

Ripoti hiyo ilieleza kuwa katika kipengele za kufanya biashara mipakani pamoja na ulipaji wa kodi, wafanyabiashara wanatumia zaidi ya saa 96 kushughulikia nyaraka zao ili kuingiza bidhaa.

Alipotafutwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, kuzungumzia ripoti hiyo, simu yale ilikuwa ikiita bila majibu.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa afagilia usafiri wa treni kwenye majiji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Russian Railways, Alexander Misharin na kumweleza kuwa Tanzania inahitaji sana kuimarisha usafiri wa ndani wa reli hasa katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Arusha, Mbeya na Tanga.

Amesema kampuni hiyo yenye uwezo mkubwa wa kujenga reli mpya, kukarabati reli, kutengeneza injini za treni na mabehewa pamoja na ukarabati wake inahitajika sana nchini ili kufanikisha mpango wa serikali wa kuimarisha reli za zamani za Tazara, Reli ya Kati na kufungua reli ya Kaskazini inayounganisha mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro na Arusha.

Waziri Mkuu alizungumza na Mkurugenzi huyo juzi katika Jiji la Sochi nchini Urusi, ambapo alitumia fursa hiyo kuikaribisha kampuni hiyo kuwekeza nchini hususan katika sekta ya ujenzi, ufundi na mafunzo ikishirikiana na kampuni za Watanzania.

"Katika kipindi hiki ambacho Tanzania inajenga reli ya kiwango cha kimataifa ya SGR pamoja na kufufua reli ya Kaskazini, inaikaribisha Kampuni ya Russian Railways kwa mikono miwili ije ifanye mazungumzo rasmi na wizara husika. Pia serikali inao mkakati wa kujenga reli mpya katika ukanda wa kusini kutoka Mtwara hadi Ruvuma ili kuiunganisha Bandari ya Mtwara na mikoa ya Kusini pamoja na nchi jirani za Malawi na Zambia."

Alisema Tanzania inahitaji sana kuimarisha usafiri wa ndani wa reli hasa katika majiji hayo, hivyo endapo mazungumzo kati ya wizara husika na kampuni hiyo yataonekana kuwa na tija na yana maslahi kwa Watanzania, kampuni hiyo itapewa fursa ya kuwekeza nchini.

Kadhalika, Waziri Mkuu aliwakumbusha wafanyabiashara wa Tanzania, wito wa Rais Magufuli wa kuwataka watumie fursa lukuki zilizopo nchini kuanzisha kampuni za pamoja na kampuni za nje ili kuunganisha nguvu kwa kuendesha kwa pamoja kampuni zitakazoanzishwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Russia Railways, Misharin, alimhakikishia Waziri Mkuu kuwa kampuni yake iko tayari kushirikiana na wafanyabiashara wa Kitanzania katika kuanzisha kampuni za pamoja ili kuipatia Tanzania teknolojia ya masuala ya reli na kubadilisha ujuzi.

Awali, Waziri Mkuu alizungumza na wakurugenzi wa kampuni ya kutengeneza matrekta ya BTP, Alexsey Punkov na Ignat Dydyshkoa, ambaye alisema kampuni yake inakusudia kuwekeza Tanzania katika sekta ya kilimo kwa kuleta nchini mashine mbalimbali kama vile matrekta na mitambo ya ujenzi wa barabara.

Viongozi wote wa kampuni za Urusi waliozungumza na Waziri Mkuu waliahidi kuja Tanzania mwaka huu ili kujionea fursa za uwekezaji na kufanya mazungumzo yenye lengo la kushirikiana na wafanyabiashara wa Kitanzania katika uwekezaji wao wanaokusudia kuufanya nchini.

Majaliwa pia alizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Zarubezhnefe, Sergey Kundryashov ambaye alionyesha nia ya kutaka kuwekeza nchini.



Wakazi wa Kijiji cha Nyaminya mkoani Mara, wakishusha mifuko ya saruji iliyotolewa na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo (hayupo pichani), juzi, zikiwamo fedha taslimu 300,000/- na milango mitatu kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Shule za Msingi za Nyaminya A na B. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Watakiwa kufanyia kazi matokeo utafiti wa mifugo

**Na Futuna Seleman,**

**DODOMA**

WATAFITI nchini wametakiwa kuyatumia matokeo ya utafiti wa mifugo wanaofanya kuwasaidia wafugaji kwa kufanya majaribio ya matokeo yake.

Lengo ni kuthibitisha kazi za matokeo ya utafiti huo hususan maeneo ya vijijini walengwa badala ya kuzihifadhi kwenye makaratasi.

Aidha, wafugaji nao wametakiwa kutumia matokeo ya tafiti za watafiti nchini ili waweze kunufaika nazo kwa kuwa na mifugo bora na kuzalisha bidhaa zenye ubora kutokana na rasilimali mifugo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Mifugo Tanzania (TALIRI), Dk. Elig Shirima, aliyasema hayo katika kongamano lililowajumuisha wataalamu wa mifugo nchini na nchi jirani zaidi ya tano wakiwamo watafiti lililofanyika jijini Dodoma chini ya ufadhili wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

"Utafiti kama kupika chakula na kupika ili kiwe na ladha, ni lazima upate mlaji na walaji wa teknolojia ni wafugaji kwa hiyo sasa hivi baada ya kurekebisha majarida tunawasiliana na Tamisemi na kutekeleza mradi majaribio hayataishia katika makaratasi," alisema na kuongeza kuwa:

"Tutakwenda vijijini kufanya majaribio baadhi ya matokeo mengine unayapata ndani ya kituo, lakini kumbe unapofika kwa mfugaji au kijijini inaweza ikawa hivyo ama tofauti, lakini ili mradi unamajibu unaweza kuthibitisha zaidi."

Alisema asilimia 75 ya Watanzania wanategemea sana shughuli za kilimo ambacho kitatoa ajira kwa Watanzania kutokana na malighafi nyingi zinatokana na mifugo na mifugo, hivyo ni lazima zitoe tija kuelekea uchumi wa viwanda kwa kuzalisha bidhaa bora.

Alisisitiza matokeo ya utafiti huo yapatikane katika mitandao mbalimbali makongamano kupita vyombo vya habari kikubwa ziwafikie wananchi ambao ndio walengwa.

"Bila kuzitangaza hakuna kazi iliyofanyika moja ya kipimo cha mtafiti ni kumpima kutoa taarifa zake kwa njia ya mikutano, majarida ya kitaifa kuongea katika vyombo vya habari," alisema Dk. Shirima.

Naye Mtafiti Mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Thabita Kintingu, akielezea utafiti wa kisayansi kwa wafugaji kujua wanapenda tabia zipi za kuku wa kienyeji na walioboreshwa, wamebaini wanawake wanapenda tabia za kuku wanaotaga mayai mengi ili waweze kupata chakula kwa ajili ya familia na kuboresha afya ya familia hususan kwa watoto.

## Pwani yapigia debe uwekezaji viwandani

**Na Mwandishi wetu,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amepongeza uwekezaji uliofanywa na katika kuchagiza Pwani ya viwanda kwa kutoa mikopo katika miradi yenye tija na maendeleo mkoani humo.

Mhandisi Ndikilo aliyasema hayo wakati alipotembelea kushuhudia miradi iliyowezeshwa na benki hiyo wakati wa maonyesho ya wiki ya viwanda yaliyokuwa yakifanyika mkoani humo.

Mhandisi Ndikilo alisema kuwa uwekezaji wa Benki ya Maendeleo (TIB) umechangia kwa kiasi kikubwa katika kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhamasisha shughuli za uwekezaji katika viwanda.

"Tumeshuhudia uwekezaji ulivyoleta manufaa mkoani kwetu hali inayochagiza shughuli za maendeleo hasa katika kutoa ajira mkoani Pwani," alisema.

Mkuu wa Mkoa aliongeza kuwa uwepo wa benki ya hiyo mkoani Pwani kumechangia kwa kiasi kikubwa kutekeleza kwa vitendo lengo la Serikali ya Awamu ya Tano ya kuchagiza Tanzania ya Viwanda. Aliongeza kuwa benki ya hiyo imekuwa sehemu muhimu ya utekelezaji wa uchumi wa viwanda kwa kuwa kichocheo cha kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi hususani kwenye maeneo yenye viwango hatarishi vikubwa.

Aliyataja mafanikio yaliyoletwa na uwekezaji wa benki hiyo ikiwamo uwezeshaji wa kampuni ya uzalishaji kuku ya Mkuza na Kampuni ya Vifungashio ya Global zilizopo mkoani Pwani.

"Tunawashukuru sana kwa kuwawezesha watu wa sekta binafsi ambao kwa hakika tunawashuhudia wanavyofanya vizuri mkoani Pwani," aliongeza.

Baadhi ya wanufaika wa mikopo hiyo ambao wako mkoani Pwani wamesema mikopo iliyotolewa na benki ya hiyo imewezesha kuongeza tija na uzalishaji hali inayochangia kuongeza uwekezaji na kutoa ajira kwa Watanzania.

Mmoja wa wakurugenzi wa kampuni ya Mkuza, Doreen Maximambali, alisema mkopo uliotolewa na benki hiyo imewezesha kubadilisha mfumo wa uzalishaji kutoka uzalishaji wa mikono hadi uzalishaji wa kutumia mitambo inayojiendeshea yenyewe.

Naye Adoh Mapunda, mtaalamu mwelekezi Kampuni ya Global Packaging inayojihusisha na uzalishaji wa vifungashio, alisema mkopo huo umesaidia kuongeza uzalishaji wa vifungo bora ambavyo vimevutia wateja kutoka ndani na nje ya nchi hali inayoongeza kipato na kodi kwa serikali.

## Wauza majisafi Dar watambulika

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa), imeanza mpango wa kuwatambua na kuwasajili kwa kuwapatia cheti cha utoaji huduma za majisafi wauza maji ya visima virefu vilivyopo pembezoni mwa mji ambapo mtandao wa Dawasa haujafika.

Taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Uhusiano kwa Umma ya Dawasa, ilisema mamlaka hiyo ndicho chombo kilichokasimiwa kisheria kusimamia huduma za usambazaji majisafi ndani ya eneo lake la huduma ambalo ni Jiji la Dar es Salaam na miji ya Mlandizi, Kibaha, Bagamoyo, Kisarawe na Mkuranga mkoani Pwani.

"Ili kutimiza takwa hili la kisheria, Dawasa imeanza kuwatambua na kuwasajili kwa kuwapatia cheti cha utoaji huduma za majisafi watoa huduma za maji kupitia visima virefu ndani ya eneo inalohudumia ili kufanikisha zoezi hili wauzaji wa majisafi kwa kutumia visima waliopo jijini Dar es Salaam wanatakiwa kufika katika ofisi za Dawasa zilizopo Gerezani kuanzia Oktoba2 8, 2019 kwa ajili ya kutambuliwa," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Watoa huduma watatakiwa kuwa na taarifa za wateja wanaowahudumia, vyeti vya ubora wa maji na taarifa za visima na kwamba katika zoezi hilo Dawasa haina tozo yoyote kwa wenye visima.

"Dawasa inapenda kusisitiza kuwa dhumuni la zoezi hilo ni utambuzi wa watoa huduma katika Jiji la Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji huduma za majisafi kwa wananchi na si vinginevyo.

Utoaji vyeti utafanyika kwa mwezi mmoja baada ya tangazo hilo, na kuwa na baada ya muda wa kusajili kupita, mtoa huduma yoyote asiye na cheti cha kutoa huduma hataruhusiwa kuuza maji.

# Udhuru wa hakimu wapiga kalenda kesi ya Kabendera

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepiga kalenda kesi ya inayomkabili mwandishi wa habari, Erick Kabendera ya uhujumu uchumi ikiwamo kuongoza genge la uhalifu na kutakatisha fedha wa zaidi ya Sh. milioni 100, mpaka Novemba 7, mwaka huu.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Vick Mwaikambo baada ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile kuwa na udhuru wa kikazi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado unaendelea na kwamba hakimu anayesikiliza kesi hiyo amepata udhuru. Wakili wa utetezi, Regnald Martin ,alidai kuwa hawana hoja mpya wanasubiri tarehe nyingine kesi hiyo itakapokwenda mbele ya Hakimu Rwizile.

Hakimu Mwaikambo alisema kesi hiyo itatajwa Novemba 7, mwaka huu na mshtakiwa apelekwe mahabusu.

Awali, wakili wa utetezi Jebra Kambole alidai kwamba Kabendera anakusudia kuanza majadiliano na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ya namna ya kumaliza kesi inayomkabili.

Katika kesi ya msingi, Kabendera anadaiwa katika siku tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 2019 katika maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, alitoa msaada katika genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Pia anadaiwa bila kuwa na sababu za msingi kisheria alishindwa kulipa kodi ya Sh. 173, 247,047.02 ambayo ilitakiwa ilipwe kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Shtaka la tatu anadaiwa mshtakiwa alijipatia Sh. milioni 173.2 wakati akijua kuwa fedha hizo ni za kutakatisha na zao la makosa tangulizi ya kukwepa kodi na kujihusisha na genge la uhalifu.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.



Wasamaria wema wakijaribu kulinasua gari lililokwama kwenye dimbwi la maji yaliyotuama barabarani katika eneo la Kitunda, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wadaiwa sugu sasa waundiwa mfumo wa kuwadhibiti

**Na Enok Charles**

KATIKA kudhibiti wakopaji wasumbufu, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imezindua rasmi kanzidata itakayowezesha upatikanaji wa taarifa za fedha kwa wakopaji kwa lengo la kuwatambua wafanyabiashara wanaokopa na kushindwa kurejesha kwa wakati.

Benki Kuu imezindua kanzidata hiyo kwa kushirikiana na Dun & Bradstreet Credit Bureau Tanzania Ltd. Akizungumza katika uzinduzi wa mfumo huo jijini Dar es Salaam juzi, Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Fedha kutoka BoT, Jerry Sabi, alisema mfumo huo ni mapinduzi mapya ya kuwezesha taasisi za fedha kutoa mikopo kwa wingi. Alisema BoT imeshatoa leseni kwa kampuni hiyo ili kuchakata taarifa za wakopaji kutoka kwenye kanzidata ya Benki Kuu.

Naye Ofisa Mkuu Mtendaji wa Dun & Bradstreet Credit Bureau, Miguel Llenas, alisema kuwa mfumo huo utasaidia benki na taasisi zinazotoa mikopo kuwatambua wakopaji wasumbufu na kupunguza mikopo chechefu.

Alisema mfumo huo pia utaongeza uwajibikaji katika kukopesha na kukopa, pia utasaidia wakopeshaji na wadai kusimamia vitabu vyao vya mkopo na kuhakikisha viwango vya riba hulingana na maelezo husika ya mkopaji na kukuza bidhaa za mkopo katika soko la wakopeshaji.

"Pia inapunguza muda wa kupata mkopo kulingana na taarifa za mkopo zilizopo kwenye ripoti zake hivyo kuwawezesha kama dhamana ya mkopo wako mpya na kukupatia mkataba bora na wenye kiwango stahiki cha riba.

"Inampa mkopeshaji taarifa sahihi za mchakato wa utoaji wa mikopo; ujumbe na mwongozo wa tathmini ya mkopaji, pia kuwezesha kasi ya utoaji mkopo na usimamizi wa wateja husika.

"Pia mtoaji wa huduma anaweza kuongeza kasi ya upatikanaji wa wateja, kuelekeza na kusimamia mipaka ya mkopo yao na kuboresha utoaji wa huduma hizo.

Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Adebowale Atobatele, alisema lengo lao kila wakati limekuwa kutoa suluhisho la usimamizi kuelekea mikopo isiyolipika katika sekta mbalimbali na kutoa taarifa sahihi kwa watoa mikopo kufanya maamuzi sahihi ya kutoa au kutokutoa mikopo.

"Lakini kuharakisha kasi yao ya kuchukua maamuzi; kurahisishaji upatikanaji wa haraka wa bidhaa za mikopo kwa kampuni zinazostahiki, watu binafsi na hivyo kukuza fursa za ukuaji kwa uchumi kwa wote.

"Pia tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na wadau wote na wahusika wote nchini ili kusaidia kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za mkopo nchini, "alisema.

Alisema kanzidata hiyo itakuwa na taarifa za kihesabu ambazo wakopeshaji hutumia, pamoja na ripoti ya mkopo kutathmini hatari ya kutoa mkopo.

"Mfumo huu ni njia muhimu za kukopesha ambayo inaweza kuamua ikiwa unapata mkopo, viwango gani vya riba unalipa kwa deni husika," alisema.

Naye Ofisa Mkuu wa Masuala ya Ufundi, Kelyn Pena, alisema mfumo huo kwa watumiaji wa kampuni hiyo wa kipekee nchini Tanzania kwa sababu inatoa taarifa halisi za kitakwimu.

# Chadema wajipanga kuweka wagombea kila kijiji, vitongoji

**Na Allana Isack,** MANYARA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) mkoani Manyara, kinatarajia kusimamisha wagombea wa uenyekiti na wajumbe wa serikali ya vijiji, mitaa na vitongoji vyote kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa wa Novemba 24, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Chadema wa Mkoa wa Manyara, Gervas Sulle, akizungumza na waandishi wa habari wilayani Mbulu, alisema hakuna eneo la kijiji au kitongoji kitakachowachwa wazi ya bila kusimamisha mgombea wa Chadema.

Sulle alisema japokuwa bado hawajapanga tarehe maalum ya kufanya uchaguzi wa kura za maoni, lakini wamejipanga kugombea katika maeneo yote. Alisema wameshatoa taarifa ya kuanza kwa mchakato wa kura za maoni ingawa hawajaweka tarehe rasmi lini zoezi la kuchukua fomu za kugombea litafanyika.

Hata hivyo, alikanusha taarifa za uvumi mitaani kuwa wanasubiria wagombea watakaoenguliwa kwenye kura za maoni kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) ili wawapatie nafasi ya kugombea kwa Chadema. "Sisi tumejikamilisha tuna wagombea wetu kamili ambao wataiwakilisha Chadema bila kusubiri makapi kwa wagombea ambao wameshindwa CCM," alisema Sulle. Alisema wamejipanga kuhakikisha kila kitongoji, mtaa au kijiji kwenye mkoa huo, wanakuwa na wagombea wao kupitia chama hicho.

"Huu mpango wa kusema eti kuna mgombea wa CCM atapita bila kupingwa na wagombea wa Chadema hawatagombea hiyo siyo kweli na tutajipanga kwa ushindani kwenye uchaguzi huo," alisema Sulle.

Alitoa wito kwa wanachama wa Chadema kutumia fursa hiyo kujitokeza kwa wingi ili kugombea nafasi mbalimbali za serikali za mitaa kwenye uchaguzi huo. Diwani wa Uhuru Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Felisi Manimo, alisema chama hicho kimejipanga kushinda viti vyote vya uenyekiti wa vijiji na vitongoji mkoani humo. Manimo alisema wananchi bado wana imani kubwa na chama hicho na wana uhakika watawapigia kura uchaguzi wa mitaa.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Qatesh wilayani Mbulu, alipowatembelea jana.
**PICHA: GIFT THADEY**

# Mnyeti ampa mtihani mkandarasi

**Na Allan Isack,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amempa mtihani mkandarasi wa kampuni ya Gopro Construction Ltd, kukamilisha kwa wakati ujenzi wa barabara ya Mbulu mjini kwa kiwango cha lami.

Mnyeti alimwambia mkandarasi huyo kuwa kama akikamilisha ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa mita 500, yupo tayari kumwongezea kipande kingine cha ujenzi wa barabara yenye urefu kilomita 0.5.

"Mkandarasi kama ukifaulu mtihani wa kutengeneza barabara hii ya mita 500 kwa kiwango cha lami na ikamilike kwa wakati nipo tayari kukupa tenda ya kujenga barabara nyingine yenye urefu wa kilomita 0.5 kwa kiwango cha lami," alisema Mnyeti.

Akizungumza wakati wa kukagua ujenzi wa barabara hiyo, Mnyeti alisema ujenzi huo upo katika hatua za mwanzo na matarajio yake ujenzi utakamilika kwa wakati.

"Hakikisheni mnachapa kazi usiku na mchana mradi huu ukamilike kwa wakati ili niweze kuwaletea fedha nyingine za kujenga mradi mwingine, siyo tunaleta fedha nyingi halafu zinakaa bure bila ya kutumika," aliongeza Mnyeti.

"Barabara hii tengenezeni kwa kiwango kinachotakiwa ili mpate tenda nyingine ya ujenzi, lakini mkiharibu mimi sitakubali kuwapa tena tenda mfano mzuri manaweza kuupata kwa mkandarasi wa Babati baada ya kukamilisha ujenzi wa awali tulimwongezea tena."

"Nimewaagiza Tarura wampe kipande kingine cha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilichobakia kwa sababu amefanya mambo mazuri kama ilivyokuwa matarajio yetu sisi kama serikali," alisema Mnyeti.

"Sasa tunakupa mtihani huu wa kwanza jenga barabara hii ya mita 500, kwa kiwango cha kinachotakiwa na kwa spidi inayotakiwa na ukifaulu kutekeleza hilo, tutakuongezea barabara nyingine," aliongeza Mnyeti.

# Wajawazito washauriwa milo kamili

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WANAWAKE wanaojiandaa kuzaa wameshauriwa kula mlo kamili, kabla ya kubeba mimba na baada ya kubeba mimba, ili kuimarisha afya kwa ajili ya kumsaidia mtoto tumboni aishi vizuri.

Ushauri huo ulitolewa jana mjini hapa na Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Bernadetha Tembo, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake.

"Katika kuhakikisha tunawekeza kwa watoto tunaanza na mama anatakiwa kabla hajabeba mimba ale mlo kamili na baada ya kubeba mimba ale mlo kamili pia," alisema Tembo.

Aidha, alisema mjamzito kula mlo kamili unamsaidia atakapobeba mimba mwili uwe na nguvu za kuhimili kubeba kiumbe, ambacho huwa kikiingia mwilini kunatokea mabadiliko.

Aliyataja makundi ya vyakula ambayo yanafaa kutumiwa na wajawazito ni vyakula vya nafaka vikiwamo mahindi, mchele, viazi, ndizi za kupika, ngano na jamii ya kunde.

Makundi mengine aliyoyataja ni mboga za aina zote, matunda aina zote na mafuta na sukari.

"Mama huyu anapotumia moja ya kila kitu kilichopo katika kila kundi atapata nguvu na kupata mtoto aliye na afya bora, pamoja na kuimarisha ubongo wa mtoto," alisema.

Tembo alisema siyo mpaka vyakula vyote avitumie kwa siku moja, bali anaweza akatumia baadhi ya vyakula kwa siku.

Pia alisema kwa wanawake wanaobeba mimba wakachukia baadhi ya vyakula ajitahidi kula chakula atakachokipenda kwa wingi kwani hawezi chukia vyakula vyote.

Alisema mama mjamzito akizingatia kula vyakula vya makundi yote atamsaidia mtoto tumboni katika ukuaji wa ubongo.

Naye Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Prisca Nyaki, alisema mjamzito akikosa matunzo hasa ya vyakula vya lishe, ambavyo vinasaidia kuongeza nguvu kuna athari katika ukuaji wa mtoto tumboni.

Prisca alisema mjamzito akiwa anakula vyakula kama mihogo, ugali na vyakula vingine vya kumpatia nguvu, hata muda wa kujifungua ukifika hawezi kupata shida atajifungua vizuri.

Taabu Kelvin, mkazi wa Babati, alisema mjamzito akikosa chakula cha uhakika na chenye lishe, ujauzito atauona kuwa ni mzigo badala ya kufurahia.

Huruma Imani, alishauri wataalamu wa lishe kuongeza kasi ya kutoa elimu ya lishe ili iwasaidie wanawake na kuepuka gharama zingine ambazo wanaweza kuingia wakipata matatizo ya kukosa elimu.

# KKKT yatangaza mambo makubwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KATIKA jitihada za kuongeza nguvu kwenye biashara ya usafirishaji wa bajaji, Saccos ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, imeanza kutoa mikopo ya bajaj za biashara.

Hatua hiyo, inakuja baada ya usafiri wa bajaj kuyazidi kete mabasi madogo (Hiace), kwenye kusafirisha abiria mitaani.

ELCT-ND Saccos, imeanza kutoa mikopo ya bajaj za biashara ya abiria ili kuwawezesha wanachama wake kujiinua kiuchumi.

Mtendaji Mkuu wa ELCT-ND Saccos , Monica Mlay, alisema ujio wa mikopo hiyo ni fursa ya kiuchumi kwa vijana walio na ndoto za kuwa wafanyabiashara wakubwa wa sekta ya usafirishaji siku zijazo.

"Ni vizuri wakajitokeza kwa kwingi na kujiunga na chama hiki ili waweze kunufaika na fursa mbali mbali za mikopo inayotolewa kwa riba nafuu. Huwezi kukabiliana na umasikini kwa kusubiri kuajiriwa au kungoja neema ya Mungu ukiwa umekaa nyumbani ama kijiweni, ni vyema ukope," alisema Mlay.

Mbali na mikopo ya bajaj, chama hicho pia kimeanza kutoa mikopo ya bodaboda na matrekta kwa ajili ya kilimo na shughuli nyingine za uzalishaji.

Alisema chama hicho kimeamua kununua na kutoa mikopo ya vifaa halisi ili watu wakope hadi mara tatu kulingana na akiba zao.

Pamoja na mambo mengine, Saccos hiyo imeeleza kuwa imeanza mchakato wa kuandaa mpango wa kutekeleza mradi wa kujenga nyumba za gharama nafuu utakaokuwa na unafuu huo kwa wateja mbalimbali.

"Tupo kwenye maandalizi ya mwisho, baada ya mazungumzo na KKKT, makao makuu yaliyopo Arusha, tunakamilisha mradi wa viwanja na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

"Tuliona ni lazima tubuni mbinu rahisi za kujenga nyumba bora ambazo zitauzwa kwa gharama nafuu kuliko zinazouzwa sasa ambazo wananchi wengi wanashindwa kuzinunua kwa sababu bei yake ni kubwa mno na wengi wana kipato kidogo," alisema Mlay.



Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (kulia), akionyeshwa aina ya noti bandia na ofisa mmoja wa Benki Kuu ya Tanzania, Kanda ya Arusha, wakati wa mkutano wa kutoa elimu uliofanyika kituo cha mabasi cha Bomang'ombe, wilayani humo mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Waonya kitisho cha kuchezea viuavijasumu

**Na Godfrey Mushi,** KILIMANJARO

MATUMIZI mabaya ya viuavijasumu (antibiotics) yanawaweka kwenye hatari takribani watu milioni 10 nchini, ambao watakabiliwa na tatizo la kukosa tiba sahihi, kufikia mwaka 2050.

Imeelezwa kuwa hatari hiyo inatokana na kuongezeka kwa matumizi ya dawa za kupambana na vimelea vya magonjwa za viuavijasumu.

Hatari hiyo inatajwa kusababishwa na usugu wa dawa mwilini, hasa kutokana na watu kutokufuata ushauri wa wataalamu wa afya na wakati mwingine kutumia dozi nusu au vidonge vichache.

Angalizo hilo ni kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa na Taaluma ya Kilimanjaro (KCRI) katika Hospitali ya Rufani ya KCMC, Dk. Blandina Mbaga.

Katika taarifa hiyo, aliyoitoa jana, wakati wa kongamano la elimu kwa wataalamu wa tiba na uuguzi, alisema matumizi mabaya ndiyo chanzo cha usugu huo. Kongamano hilo la siku moja lilikuwa na mada kuu mapambano dhidi ya usugu wa viuavijasumu.

Kwa mujibu wa Dk. Mbaga, tatizo la usugu wa dawa kwenye miili ya watu wengi kwa sasa, linatokana na kushindwa kupima afya ili kupata tiba sahihi na badala yake hujikuta wakinunua dawa kwenye maduka ya mitaani na kuzitumia.

"Kama hatua hazitachukuliwa kudhibiti wimbi hili la wananchi kununua dawa mitaani, bila kufuata ushauri au vipimo kutoka kwa wataalamu, kuna hatari kubwa ya watu kupoteza maisha kwa kukosa tiba," alisema mtafiti huyo. Wakati wa kongamano hilo, baadhi ya wataalamu wa tiba wakichangia mada ya usugu wa 'antibiotics', walieleza namna matumizi yake yanavyoweza kuacha sumu mwilini.

Akichangia mada hiyo, Mfamasia Mkuu wa Serikali, Dk. Daud Msasi, alisema kutokana na ukubwa wa tatizo hilo, tayari serikali imeandaa muswada wa sheria utakaopelekwa bungeni wakati wowote ili kutunga sheria, kwa ajili ya kuzuia wenye maduka ya dawa za binadamu kutoa dawa kwa wananchi, bila uthibitisho wa daktari.

Aidha, baadhi ya wataalamu akiwamo Dk. Sara Urassa, Mkurugenzi wa Huduma za Tiba wa Hospitali ya Rufani ya KCMC, alisema elimu zaidi inahitajika kwa wananchi.

Aliongeza kuwa tatizo la matumizi ya dawa za kupambana na vimelea vya magonjwa hapa nchini ni kubwa.

"Kutokana na kuwapo kwa idadi kubwa ya wagonjwa wanaofika hospitalini kushindwa kutibiwa kwa wakati kutokana na usugu wa dawa mwilini, ni vyema watu wakawa makini na matumizi ya viuavijasumu. Kutumia dawa bila kufuata ushauri wa daktari ni hatari kwani hutengeneza sumu mwilini, kwa sababu dawa hizo huwa zina kemikali sumu ambazo hupambana na vimelea vya magonjwa," alieleza zaidi Dk. Furaha Lyamuya ambaye ni daktari bingwa wa magonjwa ya ndani na kuambukiza.

# Vigogo wanaong'ang'ania West Kilimanjaro kutajwa

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MALALAMIKO ya wananchi dhidi ya idadi kubwa ya viongozi wa serikali na watendaji wa umma wanaoshindana nao kugombea, vitalu kwenye shamba la miti la taifa la West Kilimanjaro, yanafanyiwa kazi.

Vigogo hao wanataka vitalu hivyo kwa ajili ya kilimo kwenye shamba la miti la West Kilimanjaro.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alipoulizwa jana na Nipashe kuhusu madai hayo alisema bado ofisi yake inafuatilia suala hilo na ikikamilisha ripoti yake ya uchunguzi itaiwasilisha kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira.

"Bado kazi haijakamilika, kwa sasa tunashughulika na maandalizi ya uchaguzi ujao wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, nadhani tutakapomaliza na kazi hiyo tutashughulikana na hayo ya West Kilimanjaro," alisema.

Malalamiko ya wananchi kuhusu viongozi hao wa umma na baadhi ya watendaji kupishana na wananchi katika kugombania vitalu vya kilimo, yalitolewa katika mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Mkoa, siku kadhaa zilizopita na mwanakijiji mmoja.

Mlalamikaji huyo Azaria Mdoe, mkazi wa Kijiji cha Matadi, kilichopo Kata ya Endumeti, Wilaya ya Siha, alilalamika kwa Mkuu wa Mkoa.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani wa mwaka 2015, Mdoe alikuwa mgombea ubunge wa Jimbo la Siha kwa tiketi ya Chama cha SAU.

Baada ya malalamiko hayo kutolewa, Dk. Mghwira, alitoa siku tatu kupelekewa majina ya viongozi wote wa serikali ambao wanashindana na wananchi kuchukua vitalu katika shamba hilo.

Mkuu huyo wa mkoa aliagiza kupelekewa majina hayo akiwa anazungumza na wakazi wa Kata ya Endumeti.

"Mkuu wa Wilaya, uko hapa, nataka uniletee majina ya viongozi waliogawiwa vitalu na wanalima mazao mbalimbali, huku wananchi wakikosa maeneo ya kilimo na mimi nitakuja kuzungumza na ninyi tena muda sio mrefu," alisema Mghwira.



Ukurasa 15

Kipunguni Dar waja na mkaa wa maboksi



Ukurasa 14

Tija kiuchumi; Matumizi 'simu janja' yanashika nafasi gani katika uzalishaji?


# BUFE

Ijumaa Oktoba 25, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 20

## 'Shida ya vijana wazito kukubali mabadiliko ya kuwatoa walipo'



# Orodha changamoto zinazoumiza wakulima pamba Kanda ya Ziwa

**Na Sabato Kasika**

KUPOROMOKA bei ya pamba katika soko la dunia, kunaelezwa kumeyumbisha wakulima na kusababisha baadhi yao kukataa tamaa na kujipanga kulima mazao mengine ya biashara.

Hilo lipo kukiwapo hitaji kwamba wakulima wa zao hilo nchini wanahitaji mazingira ya kuwakizia mapato yao kupitia uzalishaji wenye tija shambani hadi sokoni, ili waondokane na kutegemea huruma ya ongezeko la bei katika soko la dunia. Uingiliaji wa kimkakati wa juu ndio unaoweza kutatua mgogoro wa kuanguka bei kwa muda mfupi na mrefu, ili kutojirudia vikwazo kila mara na utaendeleza ushindani wa pamba kwa ajili ya viwanda vya ndani na vya nje.

**MADIWANI**

Diwani wa Kata ya Matongo, wilayani Meatu, Ng'adida Tuyi, anasema pamba ni kimbilio la wakulima wao ambao baada ya mavuno matarajio yao ni kununua mifugo na mashamba.

INAENDELEA UK.18

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Mradi unaozuia ng'ombe kufa, huwanenepesha, majosho kibao

Ukurasa 16

BIASHARA

# Tija kiuchumi; Matumizi 'simu ja yanashika nafasi gani katika uza



**Na Nimi Mweta**

WATAALAMU wa umma wanasema kuna zaidi ya simu milioni 20 nchini zinazounganishwa na mtandao wa kimataifa au lugha ya kawaida ya intaneti 'worldwide-web'.

Baadhi ya wazungumzaji wanajadili takwimu hiyo katika mtazamo kwamba wapo watu milioni 20 walio katika mawasiliano ya mitandao kimataifa.

Ni mpangilio wa tafsiri ya takwimu inayojitokeza, pia katika maeneo ikitafsri katika namna, mathalani watu wangapi wana simu nchini, badala ya kudadisi au kutoa takwimu idadi ya simu zimeuzwa nchini na zinabadilishwa kwa kiwango gani.


Siyo rahisi kusema ni watu milioni 20 wana simu tena zilizounganishwa kwenye mtandao. Ni ngumu kidogo kujumuisha kirahisi kwamba zaidi ya nusu ya Watanzania wameingia kwenye mfumo wa intaneti.

Ziko takwimu zinazorejewa kila mara, kwamba zaidi ya nusu ya Watanzania wako katika umri wa ujana, yaani hawajavuka miaka 35.

> **Mfano, ni namna gani mtendaji anaweza kuwa katika sehemu ya kazi, ilhali nyumbani katika familia kuna shida kubwa, kama vile kuuguliwa.**

Mawasiliano tofauti ya mtandao kupitia simu na kompyuta, yakiendelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO**





# nja’ lishaji?





Vivyo hivyo, kati yao kuna kundi kubwa ni vijana na watoto ambao hawajavuka miaka 15.

Pia, wapo wanaoelezwa kuwa na umri zaidi ya miaka 50, hasa vijijini na hasa kinamama wasio na mawasiliano binafsi, ila wanapitia kwa wanafamilia na aghalabu wanaendelea na shughuli za uzalishaji mali au kuhusika na mali kwa njia tofauti.

Hata kama kundi hilo la wazee wasio na mawasiliano binafsi siyo kubwa, bado linapunguza uwezekano wa kuwapo watu wanaotajwa ni milioni 40 wana simu na kati yake, milioni 20 wameunganishwa na mtandao, ikichukuliwa ni idadi ya simu.

**MATUMIZI MITANDAO**

Jambo la msingi liliongelewa katika utangulizi wa kufanyika mkutano wa mwaka kuhusu matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, ni kwamba sehemu kubwa ya mitandao hutumika kwa mahitaji ya kijamii na siyo zaidi kiuchumi.

Wapo wataalamu wanaodai mitandao ni mahali tu pa gumzo na siyo kujifunza kipya au kuongeza tija katika eneo la uzalishaji na biashara. Hiyo inamaanisha kuwapo Watanzania wanaoweza kukosa faida lukuki za mawasiliano katika mitandao yao.

Kuwapo hisia iliyojengwa kutoka kwa baadhi ya Watanzania ni ‘mbumbumbu’ wa matumizi yakinifu na yenye tija wanapotumia mitandao, inaendana na swali ni nini nafasi ya tija ya mitandao, hasa inapotokea kutumika pasipohusika au eneo la ziada.

Jumuisho hilo la kitafiti ni kwamba, matumizi ya teknolojia ya mawasiliano kwa ‘simu janja’ hayana tija kubwa kiuchumi, zaidi tu ni kupeana habari nyepesi za vikundi tofauti vya ‘kula na kunywa.’ Kumeshatolewa maoni ya picha ya umma ya kitafiti, ambayo inaacha maswali juu ya usahihi wake. Utafiti, uliolenga matumizi ya ‘simu janja’ na kiwango chake cha tija katika uzalishaji kinachoweza kutazamiwa.

Kimsingi, majibu chanya kuhusu faida au tija ya kutumia mitandao kwa mawasiliano, inapaswa kuchimbuliwa katika maeneo kadhaa, kama vile kutafuta ukweli wa kiwango gani misaada ya haraka kwa masuala ya ugonjwa au tatizo jingine katika familia, hutegemea matumizi ya simu yenye mtandao?

Kuna vikundi vya kiushirika na kusaidiana au vya kuunda kazi za pamoja, wanaunda ukurasa wa pamoja (ndiyo hiyo WhatsAp - maana yake ‘what is up’ au kuna nini?) kupashana habari, kwa mfano muda halisi wa kufanya mkutano na kama kuna udhuru ufahamike haraka. Yote hayo ni ‘kuchati.’

Umuhimu wa kinachozungumzwa katika mfano wa maeneo tajwa, haugusi mashamba au viwanda. Kimsingi, binadamu anatakiwa ajitulize kihisia, ili afanye kazi zake kujua mwanawe amefikishwa hospitali na kupewa kitanda, ili aendelee kufanya kazi. Vinginevyo inabidi mtu aondoke kwanza.

Ni wazi, mpangilio huo katika kutumia ‘simu janja’ umeleta ufanisi mkubwa katika maisha ya kila siku, kwa kurahisisha mawasiliano ambayo yangehitaji kazi ya ziada, kwa mfano kupigiana simu za ‘tochi’ na kueleza kila kitu kwa kila mmoja.

Ni kweli upande mmoja, mtu anaweza kusambaza tangazo kama hilo kwa ‘sms’ (huduma ya taarifa fupi) lakini siyo rahisi anayetaka kuchangia suala hilo, kufanya hivyo kwa wakati unaotakiwa, au ajue mwingine anachokifikiri.

Endapo ukurasa wa pamoja katika simu (whats app) upo, kila kitu kinakuwa wazi na wahusika wanamaliza masuala hayo bila ya kuhitaji vikao, kwani hata kama ni suala la kijamii, linagusa hisia zao na wakati huo huo linainua tija zao katika shughuli wanazofanya.

Dhana nzima ya tija hata kama ya kiuchumi, haishii katika kinachofanyika kazini pekee, kwa dhana kinachofanyika mtu akiwa kazini pekee, ikigusa moja kwa moja uzalishaji mali au biashara yenye chembe ya ongezeko la thamani, kufufua fursa ya mzunguko au mlolongo wa kutoa kodi.

Dhana kamili inayosimama ni kwamba ‘mzalishaji siyo roboti’; mashine inayojazwa mafuta kwenye tangi au kutumia nishati fulani kama umeme, hailishwi chakula, ingawa inahitaji uhakika wa usalama wa wanaomzunguka kabla haijaanza kazi au inapokuwa kazini, kujua kila kitu ni chema.

Kuielewa tija kiuchumi inayotokana na matumizi ya ‘simu janja’ na mitandao, ni suala la kuzunguka kwa kiasi fulani. Mtafiti anayedadisi au kufanya kazi hiyo, anapaswa kuhoji maswali kuhusu matumizi ya kompyuta, pia habari au taarifa zenye ladha ya kushitua watu.

‘Simu janja’ huwa ni za kutumika kijamii, ingawa ina mawasiliano mengi tu ya kikazi. Suala la kuangaliwa au kushughulikia nyaraka, si mahali sahihi pa ‘simu janja’ bali nafasi ya kompyuta.

Ndiyo maana kutafuta tija katika uchumi kwa matumizi ya ‘simu janja’ ni dhana isiyo mahali pake. Tija inapatikana katika kompyuta na ‘simu janja’ inarahisishia umma kupeana taarifa.

Lakini, kama ilivyo miongozo ya fani ya raslimali watu, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kuwapo tija kazini na uhusiano bora katika sehemu hiyo na kwenda mbali hadi kwa jamii na wanafamilia wa mtendaji.

Mfano, ni namna gani mtendaji anaweza kuwa katika sehemu ya kazi, ilhali nyumbani katika familia kuna shida kubwa, kama vile kuuguliwa. Hapo ndipo inapozaa somo na nadharia ya fani hiyo kuhusu uhusiano kazini (Industrial Relationship).

# Kipunguni Dar waja na mkaa wa maboksi



Washiriki wakiangalia mkaa ambao wamefanikiwa kuutengeneza. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

**Na Yasmine Protace**

KATIKA makazi ya watu kumetawaliwa na taka nyingi, huku mijini kukitawaliwa na utaratibu wa taka katika makazi ambazo zinakusanywa na kwenda kutupwa.

Hilo linafanyika kuhakikisha, mazingira yanakuwa safi na salama. Taka hizo, baadhi ya watu wamekuwa wakichoma moto na wengine kutupa katika magari ya taka.

Pamoja na kuhangaika majumbani bila ya majibu bayana, sasa imebainika taka ni bidhaa ambayo ni rahisi kugeuzwa kuwa nishati ya mkaa.

Siku chache zilizopita, viongozi wa jumuiya ya kidini katika mazungumzo yao wameeleza azma ya kusaidiana na kuelimishana kuhusu mbinu na teknolojia ya kutengeneza mkaa, wakifunzwa namna maboksi yanatumika kutengeneza.

“Nilikuwa sijui maboksi kama yanatengeneza mkaa na baada ya kufundishwa, nimegundua kumbe hata boksi linatengeneza mkaa,” anatamka kiongozi mmoja.

Anaongeza kwamba, watu walizoea kutupa uchafu na wengine kuyachoma, sasa hiyo imechukua nafasi ya elimu mpya, maboksi yanaweza kutumika kutengeneza mkaa, jambo wanaloeleza ni wazo chanya, hata kuisaidia jamii kuacha kukata miti ovyo, hali inayosaidia ongezeko la mvua kila mwaka.

Anasema ni mazungumzo yatakayowezesha kuwaelimisha wadau wenzake kanisani katika matumizi ya nishati hiyo mbadala wa mkaa.

Sele Juma, ni mkufunzi wa mradi huo, anasema mafunzo ya kutengeneza mkaa yatasaidia makundi ya kinamama na vijana, kujiongezea kipato.

Anaeleza matarajio ya mkaa wa boksi, kwamba utasaidia kupunguza ukataji miti na watajiunga katika makundi ili ya mikopo, itakayowawezesha kununua mashine na kutanua uzalishaji wao.

Ofisa Maendeleo wa Kata ya Kipunguni, Betty Mzava, anasema anataja faida za mkaa mbadala kwa jamii, kwanza aliunga mkono hoja kutokata miti.

Anawaasa kinamama na vijana waliobahatika kupata mafunzo hayo, wasipoteze muda kuchangamkia fursa, wachukue mikopo itakayowasaidia kuanzisha viwanda vidogo vya kuzalisha mkaa.

Zuwena Jamal, mkazi wa Pugu, Dar es Salaam, ni mshiriki wa mafunzo hayo, anasema waliojitokeza kujifunza kutengeneza mkaa watafaidika, ikizingatiwa mkaa utokanao na miti una gharama kubwa na changamoto iliyopo sasa ni kujifunza utengenezaji, kabla ya kujitosa katika mradi.

Mwanaharakati wa ngazi ya jamii, Selemani Bishagazi, anasema mafunzo hayo anayotarajia yatazaa matunda kutokana na makundi mengi kujitokeza kushiriki, ikiwa ni mwendelezo wa kazi za asasi ya kijinsia, TGNP Mtandao.

Bishagazi anasisitiza ni wakati ukataji miti kupungua, kuelekea ukomo na itasaidia kuanzishwa viwanda vidogo vya kuzalisha mkaa mbadala.

UCHUMI

JICHO LA KANDA ZIWA

# Mradi unaozuia ng'ombe kufa, huwanenepesha, majosho kibao

• Buchosa, Kwimba, Misungwi, Sengerema furaha tele



Moja ya majosho yaliyopo Kanda ya Ziwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mary Geofrey**

HIVI karibuni kumekuwapo na ushirikiano kati ya serikali kuu, serikali za mitaa na wadau wa maendeleo, katika kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya wafugaji.

Ni hatua inayoendana na historia mnamo Januari mwaka jana, kulikuwapo na majosho 14 tu kati ya 103 katika Halmashauri za Buchosa, Kwimba, Misungwi na Sengerema yaliyokuwa yanafanya kazi.

Majosho, kimsingo ni miundombinu inayotumika kuogesha mifugo katika maji yaliyochanganywa na dawa kuua kupe na wadudu wasumbufu, katika lengo la kukinga mifugo na magonjwa kama vile ndigana kali, ndigana baridi na kukojoa damu.

Ni magonjwa yanayodhoofisha afya ya mifugo, yakidumaza ukuaji wao na hata kusababisha vifo. Utafiti mkubwa uliofanywa mwaka 2016 ulibaini magonjwa ya mifugo yanayosambazwa na kupe nchini Tanzania, ni hasara kubwa kwa uchumi wa nchi, ikijumuisha kiasi kikubwa cha ng'ombe wanaokufa.

Ili kuimarisha na kuongeza matumizi ya majosho, kampuni ya wataalamu elekezi na utekelezaji wa miradi ya Dalberg, ambayo imejikita katika utoaji ushauri wa mikakati ya maendeleo yenye ofisi zake jijini Dar es Salaam, inafanya kazi na serikali kupitia mradi wa Mapinduzi ya Sekta ya Kilimo.

> "
> **Tulitumia mbinu shirikishi za kutatua matatizo huku tukijifunza kutokana na changamoto tulizokutana nazo katika utekelezaji.**



Mfugaji wilayani Misungwi, akiwaingiza ng'ombe wake kwenye josho kuwaogesha dawa za kuua wadudu. Ni kati ya majosho yaliyofufuliwa kwa ufadhili wa mradi wa Dalberg 3D unaotekelezwa katika halmashauri nane za mkoa wa Mwanza.

Ni mradi unaolenga kuhamasisha mabadiliko ya kitamaduni kwenye mfumo wa kilimo kwa kuleta mifumo bora na yenye ufanisi.

Hadi mwezi Aprili mwaka 2019, idadi ya majosho yanayofanya kazi katika maeneo ambayo yametajwa kuongezeka kufikia 60 na idadi ya mifugo iliyoogeshwa katika muda wa mwezi mmoja, imeongezeka zaidi kwa idadi ya mara nne.

Kwanini hivyo? Ni mafanikio yatokanayo na usimamizi imara zaidi wa kisheria, uhamasishaji endelevu kwa wafugaji kuhusu faida za kuogesha mifugo, mshikamano wa viongozi katika ngazi zote na usimamizi mzuri wa uendeshaji na fedha.

Inaelezwa kwamba, ni mafanikio yatokanayo na shughuli za kufufua mpango wa majosho ya kuogeshea ng'ombe chini ya uwekezaji mdogo wa fedha.

Ni jambo linaloelezwa kutoa mwanga unaotengeneza maendeleo edelevu, kwa kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na serikali, kufikia mafanikio yaliko.

### OFISA MRADI

Ofisa Mradi wa Dalberg, Ines Muganyizi, anasema hali ilivyo, kwa kauli: "Tulichukulia lengo la mradi sio tu kukarabati au kujenga majosho mengine zaidi kwa ajili ya mifugo. Badala yake, tumefanya kazi kwa bidii kuhakikisha kwamba majosho ya kuogeshea mifugo yaliyopo yanatumika na wafugaji na kudumishwa kwa muda mrefu'

'Tulifanya tathmini kuweza kuelewa sababu hasa za majosho kutofanya kazi. Tulibaini kwamba, kukosekana kwa utaalamu, usimamizi mbovu wa kamati za majosho, pamoja na serikali za vijiji na utata wa umiliki ni sababu kuu.

"Sababu nyingine anazitaja ni ama kukosekana uwakilishi ama au umiliki sawa baina ya vijiji vinavyotumia miundombinu hiyo na kuharibika kwa miundombinu kutokana na kutofanyika ukarabati wa mara kwa mara," anaeleza.

'Tulishirikiana na halmashauri kuandaa shughuli mahususi zilizolenga kutatua changamoto hizo. Timu kutoka katika serikali zote nne za mitaa zilisambazwa kufanya semina za uhamasishaji," anasema Ines.

Anasema, ni semina zinazosaidia kuziba pengo la uwelewa katika jamii kuhusu manufaa ya kuogesha mifugo na inawahamasisha wakazi na viongozi wa serikali kukubali majukumu ya pamoja katika kudumisha uendeshaji majosho ya kuogeshea mifugo yao.

### KAZI YA SERIKALI

Ines anasema serikali nayo katika nafasi yake, ilijikita kutekeleza na kuimarisha mikakati, lengo ni kukabiliana na mahitaji, akitoa wa mfano wa Wilaya za Buchosa na Kwimba, timu za maofisa mifugo na ushirika, walitoa mafunzo kwa wafugaji kuhusu udhibiti wa magonjwa, usimamizi fedha na utunzaji rekodi.

Pia wilayani Misungwi, maofisa ugavi wa mifugo, walipimwa ufanisi kupitia uwezo wao wa kuhuisha shughuli za uogeshaji, sambamba na ofisa mifugo wa wilaya, aliyeteuliwa kufuatulia maendeleo ya kazi kila wiki.

Kuhusu mapengo ya udhaifu kupitia ugunduzi wa mradi, Ines anasema: "Tulitumia mbinu shirikishi za kutatua matatizo huku tukijifunza kutokana na changamoto tulizokutana nazo katika utekelezaji."

Anatoa mfano wa usimamizi mbaya wa fedha, mzizi wake ni kukosekana uwajibikaji na uangalizi wa karibu, hatimaye majosho yalifungwa kwa kukosa fedha za kununua dawa na gharama za matengenezo.

Ili kulitatua hilo, Ines anasema Halmashauri ya Wilaya Kwimba, ilianzisha mfumo wa kugawanya madaraka uliojumuisha mkataba kati ya kamati za kusimamia majosho, serikali za vijiji, na makao makuu ya halmashauri.

Vilevile anasema, walifungua akaunti maalumu benki kwa ajili ya majosho, kuimarisha uwajibikaji.

Mengine yanayotajwa ni halmashauri kusimamia sheria ndogo zinazowataka wafugaji kuogesha mifugo, jambo lililohamasisha mzunguko endelevu wa kazi na fedha za kudumisha majosho.

### OFISA MIFUGO

Ofisa Mifugo katika Halmashauri ya Wilaya Misungwi, mkoani Mwanza, Benedicta Mtolera, anasema: "Tulisambaza taarifa za mafanikio haya katika wilaya zingine pamoja na kuripoti vikwazo sugu tulivyokumbana navyo katika ngazi za mkoa na wizara.

"Ilikuwa jambo muhimu kuchukua utendaji bora kutoka kwa halmashauri za wilaya zilizofanikiwa na kupeleka katika halmashauri za wilaya nyingine ili kupata mafanikio pana zaid, kwa mwa mfano, mbinu za usimamizi wa josho zilizobuniwa na Kwimba sasa zinatumika Buchosa, Misungwi na Sengerema," anasema.

Mtolera anataja kingine ni kuwaleta pamoja maofisa kutoka Idara za Mifugo, Ardhi, Sheria, Ushirika na Maendeleo ya Jamii, iliyobuniwa kuondoa vikwazo na kuhuisha majosho na shughuli za uogeshaji mifugo, kutoka kulikothibitika kufanya vizuri kushina halmashauri nyingine

"Katika ngazi ya mkoa, timu yetu ilisaidiana na sekretarieti ya mkoa kutumia yale tuliyojifunza kuandaa mikakati rahisi ya utendaji. Sehemu ya mikakati hii inajumuisha sekretarieti ya mkoa kuunda vikosi kazi vya kufuatilia maendeleo ya utekelezaji.

"Vilevile, sekretarieti itashirikiana na halmashauri zake kubainisha vikwazo, kutambua na kutumia suluhisho zenye gharama nafuu katika kukabiliana na vikwazo hivyo," anasema Mtolera, akidai ni mbinu mkakati inayopandishwa hadui ngazi Taifa.

### MFUGAJI ALIYEFANIWA

Mfugaji kutoka kijiji cha Itumbili, katika Halmashauri ya Buchosa, Scholastica Malimi, anasema ni mabadiliko aliyoyapata kutokana na mikakati mipya kitaalamu.

"Hapo zamani, vifo vya ndama kutokana na magonjwa yanayosambazwa na kupe kama vile ndigana kali na ndigana baridi vilikuwa vingi sana.

"Mambo ni mazuri kwa sasa. Ninaweza kuogesha mifugo mara moja kila wiki na nimeridhishwa sana na matokeo, ng'ombe wangu hawana shida katika kula. Matokeo yake, uzalishaji wa maziwa umeongezeka," anasema.

Scholastica anasema, hayo yamewezekana kwa sababu ya kuongezeka ufanisi katika matumizi ya rasilimali na uwajibikaji ulioimarishwa katika usimamizi wa kupata matokeo hayo.

# Biashara katika picha



Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bia ya Serengeti SBL, Mark Ocitti akizungumza na wageni waalikwa waliohudhuria kwenye uzinduzi wa nembo mpya ya kampuni hiyo, uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, akisalimiana na mfanyabiashara wa Soko la Tandale, Juma Kihimbike, wakati alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa soko hilo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Barclays Tanzania, Simon Mponji (kushoto), akisalimiana na Makamu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kundi la Benki ya Absa, Peter Matlare, wakati wa mkutano wa masuala ya kiuchumi uliondaliwa na benki hiyo kwa wateja wake, jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa Barclays Tanzania, Abdi Mohamed. **NA MPIGAPICHA WETU**

BIASHARA

# Orodha changamoto zinazo wakulima pamba Kanda ya

• Wafunguka; wenye viwanda wanena; madiwani na

INATOKA UK.13

Anasema mwaka huu, ununuzi wa pamba umeyumba kutokana na kampuni za ununuzi kucheleweshewa fedha ambazo wananchi walitarajia kuuza pamba na kununua chakula.

"Wakulima waliuza pamba tangu Julai 23, mwaka huu, lakini hawajalipwa na wakati huo debe la mahindi linauzwa kwa Sh. 16,000 na kusababisha wawe na wakati mgumu," anasema Tuyi.

"Serikali iiangalie pamba kwa jicho la huruma, kwani inaenda kujifuta kwa ukanda wa kwetu. Iko pamba nyingi sana kwenye vituo ambavyo haijachukuliwa na wanunuzi, baadhi ya wakulima wanasusia kuuza wamebaki na pamba nyumbani," anasema.

Kuhusu ukusanyaji mapato ndani kwenye halmashauri, Tuyi anasema wajibu wao ni kusimamia ukusanyaji wa mapato ili fedha zinazopatikana ziwatengenezee wananchi miundombinu kama elimu na afya.

"Halmashauri inaweza isifikie malengo kutokana na pamba nyingi kutononuliwa, kwani nyingi bado iko nyumbani. Tunaweza tusifikie malengo na kuifanya halmashauri yetu kuyumba," anasema.

Tuyi analalamikia usumbufu kwenye usimamizi, kutokana na kampuni kutopeleka fedha kwa wakati, huku baadhi ya watu wakinunua pamba kwa njia ya machinga. Lewa Safari Magembe ni Diwani wa Kata ya Gilya wilayani Bariadi Mkoa wa Simiyu, anasema watu walilima mahindi kwa lengo la kupata chakula, lakini hawakupata chochote.

Analalamika kwamba, katika zao la pamba walitarajia kuuza ili wanunue chakula wajiwekee akiba kwa baadaye, lakini hadi sasa hawajalipwa hata kama wakilipwa ni fedha kidogo.

Anasema, watu walitarajia kununua chakula, kukodisha mashamba, kujenga nyumba, lakini baada ya fedha kukwama matarajio makusudio ya wakulima yameanguka kwa sababu mwezi wa tisa, maandalizi ya msimu wa kilimo yanapaswa kuanza, ikijumuisha kukodisha mashamba.

"Tutashindwa kufikia matarajio yetu, kwa sababu ya utoroshaji wa pamba na kampuni kutoingia moja kwa moja kwenye ununuzi wa pamba kwa wakulima," anasema.

**WAKULIMA**

Maduhu Shuguta, ni mkulima wa pamba kijijini Ng'alita kilichopo Meatu, Simiyu, anayesema ulimaji pamba unayumba kwa sababu ya malipo kukawia.

"Kiuchumi tumeathirika, kwa sababu tumeshindwa kununua chakula kwa wakati na kupeleka watoto shule. Tunaishauri serikali ibadilishe mfumo...wakulima wapate fedha na pamba inunuliwe kwa wakati," anasema Shuguta.

Maduhu Manyangu, mkazi wa Salaria-Matongo wilayani Bariadi, anasema hawajapata fedha tangu wauze pamba mwezi Julai, huku familia nyingi hazina akiba ya chakula.

Samweli Kubagwa, ambaye anaishi Salaria, ana hoja kwamba tangu msimu wa mauzo uanze mwezi Mei, wameshauza pamba, lakini hawajaliwa, hivyo anawalalamikia wanunuzi na vyama vya ushirika kuwa kikwazo cha kulipwa fedha zao.

Gomolo Lushagu, kutoka kijiji cha Matongo wilayani Bariadi, anasema wamelima pamba kwa mikopo na licha ya fedha za pamba kucheleweshwa, wanadhalilika kwa madeni.

"Mwenye deni hawezi kukuelewa, kwa sababu tulifunga mkataba kurejesha fedha mwezi wa saba, shida ya pamba ni kila mahali hakuna sehemu wanayolipa," anasema Lushagu.

Ng'hwani Edward, ni mkulima wa Matongo. Anaishauri serikali kubadili mfumo wa kilimo cha pamba kwa vile wakulima wanakata tamaa na kilimo hicho, huku wakiwa ni wa kusukumana kudai fedha zao za mauzo kila mara.

Pia Zoya Makulu, mkazi wa Mwauchumu, malalamiko yake ni



Pamba ikiwa nje katika kijiji cha Mwasengelea wilayani Meatu, ambayo bado haijanunuliwa. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**



Wakulima wakipima pamba yao katika kituo cha kukusanyia pamba kijiji cha Gibeshi, wilayani Bariadi.

**"Halmashauri inaweza isifikie malengo kutokana na pamba nyingi kutononuliwa, kwani nyingi bado iko nyumbani. Tunaweza tusifikie malengo na kuifanya halmashauri yetu kuyumba.**

# umiza Ziwa

O...





Ghala la kuhifadhi pamba katika kijiji cha Gibeshi wilayani Bariadi mkoani Simiyu, likionekana kubomoka upande, licha ya msimu wa mvua kukaribia.



kuwa athari wanayoipata ni ukosefu wa fedha, hali inayowanyima uwezo wa kununua chakula, pia kukodisha mashamba kwa ajili ya maandalizi ya kilimo msimu ujao, akidai tangu wauze mazao ya msimu uliopita, Juni mwaka huu hawajalipwa.

"Tunakosa fedha ya matibabu, kwa sababu hakuna huduma...wafanyabiashara wakubwa wametugomea, hatuwezi kusemea Amcos (vyama vya ushirika) za kwetu, kwa sababu wangekuwa wanatoa hela, tusingekuwa na tatizo," anasema Mzee Lupigila.

Anaendelea: "Leo imekuwa maumivu, hata kama una mgonjwa na umeshauza huwezi kumsaidia."

### NINI KIFANYIKE?

Mkulima Sehemu Lupigila, anasema mfumo wa ununuzi wa mwaka jana ulikuwa mzuri, kutokana na wakulima kuuuza pamba na kulipwa kwa wakati.

Anasema katika msimu uliopita soko lilikuwa zuri, licha ya mbegu za mazao zilizopatikana katika mfumo wake hazikuwa bora.

Pia anafafanua kwamba kupitia usimamizi wa mwaka jana katika uzalishaji pamba, zilipatikana mbegu bora na zilipopandwa, ziliota vizuri, kilio kimebaki kikijikita katika soko pekee.

Anasifu mkakati wa serikali kuanzisha vyama vya ushirika (Amcos) akikiri haikuwa na nia mbaya, isipokuwa anawalaumu anaowaita 'matajiri wachache' walitaka faida kuihujumu serikali.

> **"Tutashindwa kufikia matarajio yetu, kwa sababu ya utoroshaji wa pamba na kampuni kutoingia moja kwa moja kwenye ununuzi wa pamba kwa wakulima.**

"Tumefeli kwa sababu ya watu wasiokuwa na nia nzuri. Suala la pembejeo kwa wakulima awali walikuwa wanakopeshwa pembejeo, sasa waachwe wajinunulie wenyewe kwa fedha taslimu au atakayekopa ni sawa, lakini Bodi ya Pamba ijipange na iangaliwe kwa jicho la tatu, wakulima wameanza kukata tamaa na kilimo cha pamba," anasema.

"Tuweke msingi mzuri wa ununuzi wa zao la pamba, ikiwamo kuwasiliana na mataifa katika soko la dunia kabla serikali haijatangaza, bei ili kuondoa lawama, pamoja na soko kuwa chini ya Rais (Joseph) Magufuli hataki watu wake waumie, ni lazima pamba inunuliwe kwa Sh.1200," anasema.

Ngasa Magembe, mkulima wa kijiji cha Nkololo, anasema; "Kama mfumo huu utaendelea, wakulima tutakuwa hatuna haki. Hivyo, tunaishauri serikali kama imeshindwa kusimamia mfumo wa Amcos, irudishe mfumo wa soko huria tuliokuwa tunapata fedha kwa wakati, kwani tumeona hakuna kampuni inayoleta fedha kwa wakati," anasema Magembe.

### WENYE VIWANDA?

Meneja wa Kiwanda cha kuchambua pamba cha Alliance Ginnery kilichopo Kasoli wilayani Bariadi, mkoani Simiyu, Boaz Ogolla, anasema hadi sasa soko la kimataifa linaporomoka kwa kasi na kuwafanya wanunuzi wa pamba kusuasua sokoni.

"Wakati wanaanza msimu wa pamba, soko la kimataifa lilikuwa (Dola) senti 72, lakini sasa hivi soko la dunia liko senti 54, ukisafirisha pamba hadi bandarini Dar es Salaam unapewa senti 56 hadi 58, na kwa tafsiri ya haraka, mkulima anapaswa alipwe Sh. 800 kwa kilo moja," anasema Ogolla.

Meneja huyo anaomba kuingiliwa kati wanunuzi na kusimamia katika usimamizi wa bei kwa mkulima. Anafafanua: "Upande wa uchambuzi imetuathiri kwa kiasi kikubwa, kwani ilibidi tujibane na tupunguze gharama kwa kiasi kikubwa ili tuweze kuendana na hali ya soko, wakati wa makato ya bei tulipunguza gharama ya uchambuzi kutoka shilingi 138 kwa kilo hadi shilingi 130 kwa kilo moja."

Anasema, kutokana na kujibana, inaweza kupunguza uzalishaji na watumishi hawataweza kuwa na motisha, kwa vile soko liliyumba na wanunuzi wengi walisita kuingia sokoni.

Ogolla ambaye ni katibu wa wanunuzi wa pamba Babati, anasema lengo lilikuwa ni kunusuru bei ya pamba kwa mkulima ibakie 1,200.

"Kuna maeneo, ambayo wanunuzi hawakupatikana kabisa na kuna hofu kama wakulima kwenye maeneo hayo wataendelea na kilimo cha zao la pamba, kwani wamekata tamaa," anasema.

Ogolla anasema wana kazi ya ziada kwenda kuhamasisha wakulima, waone ni wakati wa mpito na mwaka unaokuja hapatakuwapo na hali kama hiyo, wanunuzi kusita kununua pamba, kutokana na kudorora soko la kimataifa.

"Inahitajika kazi ya ziada, tuwatembelee na tufanye kampeni ya kilimo cha pamba ya kutosha ili walione zao la pamba linaweza kuendelea kulimwa, uzalishaji umeongezeka kiasi kikubwa sana, soko la kimataifa kuporomoka imeathiri matarajio yao," anasema.

Anaishauri Bodi ya Pamba iende kwenye kampeni kuhamasisha wakulima, huku akikiri mwanzo kulikuwapo na siasa za watu kila mmoja aingie katika maeneo ya kuzalisha mbegu na hana uhakika watu walinunua mbegu ya pamba na kuhifadhi vizuri.

"Sisi kama Alliance Ginnery tumehifadhi vizuri na tuna uhakika itaenda kwa wakulima, lakini je, itatosha? Pia, isipohifadhiwa vizuri kuna uwezekano wa kuingia kwa mbegu chotara ambayo kila mwaka tunapigania tupate, mbegu bora inayoweza kusaidia wakulima kupata tija," anasema.

Anasema, kwa walionunua pamba hiyo maeneo ya Igunga na Meatu kama hawakuhifadhi kwa njia nzuri, hiyo mbegu isitumike, lakini kama wamehifadhi vizuri, inaweza kunusuru sekta kwa kuwa na mbegu bora.

"Kila wiki tunafanya 'Ginning Out Test' (GOT) ili kuhakikisha ina ubora kama GOT, ikipungua utajua kuwa siyo ile tuliyoitarajia kwa mkulima, lakini hadi leo uzalishaji ni mzuri, mbegu inafaa kwenda kwa wakulima," anasema.

Ogolla anahisi shida ya uzalishaji mbegu, kwa vile wakulima walizoea kukopeshwa mbegu au kupewa kwa bei ya chini na wanatakiwa kupunguza gharama, ili wahimili bei kwa mkulima ambayo inabaki kama ilivyopangwa, ili kuendeleza kilimo cha zao hilo.

Anasema, wakulima wanatakiwa kuuziwa mbegu kwa fedha taslimu na ana hofu kwa mikoa ambayo walikuwa wamezoea kukopeshwa, wakulima huenda watapata shida.

Mdau huyo wa soko la pamba, anasema serikali na wadau wanahitajika haraka, ili wapate mbegu na pembejeo kwa wakati, jinsi walivyozoea katika miaka ya nyuma.

Ogolla anawaomba wanunuzi wajitolee, kwa sababu ndiyo biashara yao, pia serikali inapaswa kuingilia haraka kuwezesha mfuko wa upatikanaji wa pembejeo.

UCHUMI

# ‘Shida ya vijana wazito kukubali mabadiliko ya kuwatoa walipo’



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu alipozungumza na makuruta katika kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Mtabila, wilayani Kasulu, mkoani Kigoma, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini katika wilaya hiyo. JKT ni moja ya maeneo ya kuwakomboa kifikra vijana. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Tatu Tambile**

VIJANA wengi nchini walioko katika ndoto ya kufanikiwa na kufika mbali, wanakabaliwa na changamoto ya ajira iliyopo nchini. Malalamiko kutoka kwa kila mtu, kupitia, dai kwamba hakuna ajira na maisha ni magumu.

Je, ni kweli hakuna ajira wala fursa ya kuweza kujiajiri kupitia mazingira yanayowazunguka?

Tunaamini kwamba kijana akijikwamua kiuchumi, jamii nzima inakwamuka, kwa kuwa vijana hao ndio nguzo muhimu katika jamii na Taifa kwa ujumla, Pia anapojikwamua, kunakuwapo na uhakika wa leo au kesho kuwa njema kwa kuwa maisha yake ‘yupo leo na kesho.’

Katika mchakato wa vijana kutimiza ndoto zao na kufikia malengo yao ya kila siku, imebainika kwamba, si sahihi kusema hakuna fursa za ajira na wala hakuna cha kufanya, ila tatizo ni kwamba vijana wengi hawaoni fursa zinazozungumzwa. Kinachodhihirika ni kwamba, vijana wanapenda sana mafanikio na wana ndoto kubwa ya mafanikio, lakini changamoto iliyopo ni wao kutoziona fursa zinazowazunguka. Badala yake, wanaishia katika malalamishi na kudai hawana kazi ya kufanya,

Je, ni jinamizi gani linalotafuna ndoto za vijana wengi na kusababisha kuua ndoto hizo zinazowazingira?

Msanii wa kizazi kipya, maarufu ‘hip hop’ na balozi wa vijana, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Wanandoto, Kala Jeremiah, amebainisha kuwa katika mustakabali wa kupata jamii bora itakayoleta matokeo chanya katika mambo yote ya kijamii, kijana anatakiwa kupata hamasa.

Anataja maeneo ya hamasa hiyo ni katika ari ya kujitambua, kutambua majukumu yao, nafasi zao na uwezo katika mambo yote ya kijamii na kiuchumi.

> “Vijana wengi hawafikii malengo ni kwa sababu wanaogopa kuthubutu kuanza. Hili jambo limekuwa la kawaida na limeua ndoto za vijana wengi.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, akipata maelezo ya mwanakikundi wa Rasupashoma Group, Ibrahim Malabela, jinsi wanavyotengeneza viatu bora. Mwenye miwani, ni Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali (mstaafu), Nicodemus Mwangela na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Vijana, James Kajugusi.

Kala anasema, utafiti waliofanya wamebaini kwamba vijana wengi wanashindwa kutimiza malengo na ndoto zao, sababu kubwa ni kuendekeza ‘kusubiria mambo yake sawa’ ndio waanze.

“Vijana wengi hawafikii malengo ni kwa sababu wanaogopa kuthubutu kuanza. Hili jambo limekuwa la kawaida na limeua ndoto za vijana wengi,” anasema.

Aidha, anawabainisha kwamba, kumekuwapo na imani potofu kuwa ili mtu afanikiwe itabidi atoke kijijini na kwenda kwenye miji mikubwa, jambo ambalo si sahihii na kujikuta wanaingia kwenye makundi ya uhalifu kama wizi, utapeli na matumizi ya dawa ya kulevya.

“Watu wanatoka vijijini wanaamini wakishafika mjini watafanikiwa. Matokeo yake, wanakutana na changamoto. Mimi naamini kuwa, kila sehemu kuna fursa za kutosha, kinachotakiwa ni kuwapa vijana mwanga wa kuziona,” anasema.

Somo lake lingine analobainisha kuwa ‘jinamizi kuu’ linalotafuna ndoto za vijana wengi na kutofikia malengo yao, ni hali ya kutojishughulisha na chochote, wakisubiri jambo fulani kutokea kuwawezesha au wafanyiwe jambo, waweze kujishughulisha.

“Tunasisitiza vijana waanze na walicho nacho. Tunaamini kuwa utajiri upo kwenye mawazo, pia nguvu alizonazo kijana ni mtaji mkubwa sana na msisitizo zaidi kwa mawazo ya kibunifu, vipaji pamoja na uthubutu,” amesema.

Kutokana na jinamizi hilo kuendelea kuangamiza ndoto za vijana ‘Kala Jeremiah’ ameamua kuanzisha kampeni iitwayo ‘Kijana Smart’ itakayolenga kuamsha hamasa kwa vijana kujitambua, kutambua nafasi zao na majukumu walio nayo.


Pia kuna suala la umuhimu wao katika mustakabali wa kupata jamii bora inatakayoleta matokeo chanya katika mambo yote muhimu ya kijamii na kiuchumi.

Ni kampeni itakayolenga kumfungua macho kijana kuona fursa zilizomzunguka katika mazingira anayoishi. Ni kampeni ya sehemu mbalimbali, ikiwamo vijijini na mijini na anasema changamoto iliyopo, ni kuwafikia vijana kupata elimu kuhusiana na kampeni hiyo.

Kipaumbele kilichopo sasa, ni namna ya kumkwamua kijana kiuchumi, kwa kumwandaa kuwa tayari kutumia vizuri akili na nguvu zake, akiibadili changamoto za jamii yake kuwa fursa, pia kuzitambua fursa mbalimbali zinazopatikana katika mazingira.

Anasema katika kufanikisha hilo, wanatumia njia mbalimbali za kutoa elimu, ikiwamo nyenzo za video, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, taasisi za elimu, shule na nyimbo.

Kala Jeremah ametoa wito kwa wadau wote kuunga mkono katika kuhakikisha wanatimiza malengo yao mazuri na yenye tija kwa jamii na taifa kwa ujumla.





Mbunge wa Jimbo la Mbarali, mkoani Mbeya, Haroon Pirimohamed Mulla, akizungumza na wananchi wa Kata za Mwatenga na Ruiwa, hivi karibuni, ikiwa ni mwendelezo wa kuwatembelea na kusikiliza kero zinazowakabili. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbaroni tuhuma za kubadilisha fedha

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

ZAIDI ya watu 20 wamenaswa na Polisi mkoani Mbeya kwenye mpaka wa Tanzania na Malawi wa Kasumulu wilayani Kyela kwa tuhuma za kufanya biashara haramu ya kubadilisha fedha.

Watu hao walikamatwa juzi wakati wa operesheni ya kushtukiza iliyofanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na maofisa wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na vyombo vya usalama ambao walikuwa wamezingira maeneo mbalimbali ya mji huo.

Katika operesheni hiyo, wafanyabiashara hao walikamatwa na zaidi ya Sh. milioni 100 ambazo zilikuwa za mataifa mbalimbali zikiwamo shilingi za Tanzania, Kwacha za Malawi na Dola za Marekani ambazo walikuwa wakizibadilisha kienyeji.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, ambaye aliongoza operesheni hiyo, alisema biashara hiyo ni haramu kwa mujibu wa sheria zinazosimamia fedha nchini.

Aliwataka wafanyabiashara hao waliokuwa wanatumia mbinu mbalimbali kuwazuga maofisa hao ikiwamo kuandika maandishi yanayoonyesha kuwa kwenye maduka yao hayo wanafanya biashara ya fedha kwa njia za simu, lakini kumbe wanafanya shughuli hizo.

"Nawashauri wafanyabiashara wote kuendelea kufuata taratibu. Mtu yeyote anayetaka kubadilisha fedha za mataifa mbalimbali anatakiwa kwenda kwenye benki zetu au kwa watu wenye vibali maalumu na sio humu wanaofanya kienyeji," alisema Kamanda Matei.

Aidha, Kamanda Matei alisema biashara hiyo inafanyika kwenye mazingira ambayo si salama kwa maisha yao, hivyo wanazipiga marufuku kwa ajili ya maisha yao.

Diwani wa Njisi, Omary Mwinjuma, alisema wananchi wa kata yake ambako walikuwa wanafanya biashara hiyo, hawana elimu ya kutosha kuhusu sheria ya fedha, hivyo akaiomba serikali kuendelea kutoa elimu.

Alisema kitendo cha kuwakamata kwa kushtukiza kitawaathiri wao pamoja na familia zao, hivyo akaomba elimu iendelee kutolewa ili kuepuka kuwakamata wengine.

"Hii biashara imekuwa ikifanyika kwa kipindi kirefu na hatukuwa na uelewa wa kutosha kuhusu taratibu mpya za ubadilishaji wa fedha, hivyo kwa sasa pamoja na kuwakamata nashauri pia elimu itolewe ili hata wananchi wa kawaida wajue maeneo sahihi ya kubadili fedha zao," alisema Mwinjuma.

Aliwataka Watanzania wanaofanya biashara kati ya Tanzania na Malawi kuendelea kufuata taratibu za nchi hizo mbili ili kuepuka kukumbana na mkono wa sheria.

# NBC yapiga jeki ujenzi kituo cha afya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imekabidhi msaada wa mifuko 600 ya saruji kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya ili kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Iyunga ambacho kilijengwa kwa Sh. milioni 400 zilizotolewa na serikali.

Msaada huo ulikabidhiwa juzi kwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, ambaye alipeleka maombi kwa benki hiyo.

Akikabidhi msaada huo, Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Salema Kileo, alisema msaada huo ni sehemu ya utaratibu wa benki kutoa sehemu ya faida na kurudisha kwa jamii ambayo ndiyo wanafanya nayo kazi.

Kileo alisema benki hiyo ina utaratibu wa kusaidia katika maeneo mengine ambayo ni elimu na wajasiriamali na kwamba kipaumbele kikuu huwa ni sekta ya afya.

"Tulifuatwa na Mwanjelwa akituomba msaada huu na sisi huwa tunaamini kuwa watu wakiwa na afya bora wanakuwa na uwezo mkubwa wa kushiriki katika shughuli za maendeleo ndiyo maana tulikubali na leo (jana) tumeamua tukabidhi," alisema Kileo.

Kwa mujibu wa Kileo, msaada huo una thamani ya Sh. milioni tisa, hivyo akawaomba wasimamizi wa mradi huo kusimamia vizuri ili ukamilike kwa kutumia saruji hiyo.

Akizungumza wakati wa kupokea msaada huo, Mwanjelwa aliishukuru benki hiyo kwa kukubali ombi lake na kukabidhi msaada huo huku akisisitiza kuwa walichokifanya ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Pamoja na kwamba msaada huo ulielekezwa kwenye ujenzi wa Kituo cha Afya cha Iyunga, kituo hicho hakitabakiwa na mfuko hata mmoja kwa sababu yeye binafsi alishatoa zaidi ya mifuko 400, hivyo itapelekwa kwenye miradi mingine.

Alisema mifuko hiyo itagawiwa kwenye miradi mingine ambayo ni zahanati ya Kalobe mifuko 100, zahanati ya Iduda mifuko 100, Kituo cha Afya cha Nzovwe mifuko 100 na mingine 300 itaelekezwa kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa na ukarabati wa baadhi ya madarasa.

Mwanjelwa alisema serikali imewekeza fedha nyingi kwenye sekta ya afya na katika Jiji la Mbeya kuna vituo vya afya viwili ambavyo vimejengwa kwa zaidi ya Sh. bilioni 1.1 na kwamba pia kuna ujenzi wa zahanati mbalimbali.

"Nawaomba wasimamizi wa miradi hii mkasimamie vizuri ili kuwaka moyo wenzetu hawa ambao wametupatia msaada huu waone matokeo chanya na siku nyingine tukiwaomba watuelewe," alisema Mwanjelwa.

Meya wa Jiji la Mbeya, Mchungaji David Mwahilindi, alimshukuru Mwanjelwa ambaye ni Mbunge wa Viti Maalumu kutoka mkoani Mbeya kwa kuwapenda wananchi wa jiji hilo ambao wamekombolewa.

Alisema pamoja na msaada huo, pia Jiji hilo linakabiliwa na uchakavu wa vyumba vya madarasa, hivyo akamwomba Naibu Waziri kuendelea kuwaomba wadau wake wasaidie.

# Nemc yapokea malalamiko 600

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc) limepokea zaidi ya malalamiko 600 yanayohusu uchafuzi wa mazingira unasababishwa na kelele kutoka kwenye kumbi za starehe, nyumba za ibada na magari ya matangazo.

Mkurugenzi Mkuu wa Nemc, Dk. Samwel Mafwenga, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Mbeya.

Dk. Mafwenga alisema malalamiko hayo yalifikishwa Nemc kuanzia Januari, mwaka huu, na kwamba wananchi wanalalamika kuwa uchafuzi huo wa mazingira umekuwa na athari kubwa kwenye maisha yao.

Alisema baadhi ya wananchi walalamika kuwa baadhi ya nyumba za starehe kama vile baa zimejengwa pembezoni mwa nyumba zao na watu wanacheza muziki usiku kucha.

Pia alisema nyumba za ibada kwenye makazi ya watu ambazo zinaendesha shughuli zake kwa kutumia vipaza sauti vyenye nguvu na kufanya hivyo hata nyakati za usiku, husababisha usumbufu mkubwa kwa watu walio jirani na nyumba hizo.

"Kelele hizo zimekuwa na athari kubwa kwa wananchi ikiwamo kusababisha uziwi kwa watu walio jirani na wanaoathirika zaidi ni watoto ambao masikio yao bado ni laini," alisema Dk. Mafwenga.

Alisema kuna kesi moja ambayo kuna mtoto aliathirika na muziki uliokuwa ukipigwa kwenye ukumbi wa starehe baada ya damu kumtoka masikioni na baada ya uchunguzi ilibainika kuwa masikio yake yalipasuka kutokana na muziki huo.

Alisema tayari Nemc imeanza kuwachukulia hatua watu wanaosababisha uchafuzi huo wa mazingira kwa kuwatoza faini na wanaokaidi wanafikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.

Dk. Mafwenga alisema faini zinazotokana na uchafuzi wa mazingira hasa huo wa kelele kwa mujibu wa sheria kuanzia shilingi laki mbili hadi Sh. milioni moja kulingana na aina ya kosa.

Alisema faini hizo zinatozwa kwa watu ambao tayari wameelimishwa na baada ya kutozwa hutakiwa kuacha kuendelea na uchafuzi huo na endapo wataendelea hatua inayofuata huwa ni kufungiwa kutoa huduma husika.

Baadhi ya wananchi waliozungumzia aina hiyo ya uchafuzi walisema kwa sasa uchafuzi wa aina hiyo unafanywa zaidi na makanisa na nyumba za starehe ambazo ziko jirani na makazi ya watu.



# Halmashauri zaagizwa kufungua akaunti maalum

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeziagiza halmashauri nchini kufungua akaunti maalum ili kuweka asilimia 10 ya fedha za mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili zisimamiwe ipasavyo na maofisa maendeleo wa jamii.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alipokuwa akifunga kongamano la wataalamu wa maendeleo ya jamii nchini. Katika kutekeleza hilo, Jafo aliagiza akaunti hizo wahakikishe zifunguliwa kabla ya Novemba 30, mwaka huu.

"Lengo la kutoa agizo hili ni kuhakikisha fedha hizo zinawafikia watu sahihi kwa muda muafaka kupitia maofisa maendeleo ya jamii kwa sababu ndio wanawafahamu walengwa zaidi kutokana na taaluma yao na maeneo wanayowajibika kiutendaji," alisema.

"Atakayeshindwa kufanya hivyo labda awe na kikwazo maalum cha kiutendaji kilichopelekea achelewe muda uliopangwa," alisema Jafo. Aidha, Waziri Jafo aliahidi kuangalia namna ya wizara yake kutenga fedha kwa ajili ya wataalamu wa maendeleo ya jamii ambazo watazitumia katika ufuatiliaji ikiwamo tathmini ya fedha hizo za mikopo.

Jafo alisema alishaagiza kufunguliwa kwa akaunti hizo lakini ameagiza tena kwa kuwa anaona halijatekelezwa.

Bila kuwa na akaunti maalum, alisema ni vigumu kuzifuatilia kwa sababu zinakuwa kama zimeingizwa kwenye jalala ambako si rahisi kuona matumizi yake.

Hata hivyo, alisema kwa kutokuwa na uwezeshaji huo kwa maofisa hao, itakuwa vigumu kwao kufuatilia uendelevu wa vikundi vilivyokopa fedha za halmashauri.

Kutokana na hilo, Jafo aliwataka wataalamu wa kada hiyo kutokuwa na hofu yoyote kwa sababu watu hao ni muhimu katika taifa kwa ajili ya kuchagiza maendeleo katika jamii.

"Naomba niahidi nitaisimamia kada ya maendeleo ya jamii kuhakikisha kila mmoja anatamani kwenda kuisomea fani hiyo. Lengo ni kuona tunakuwa na maofisa maendeleo ya jamii wengi," alisema Jafo.

Katibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. John Jingu, alisema anaamini baada ya mkutano huo, maofisa maendeleo ya jamii watakwenda kufanya mabadiliko na kuleta maendeleo katika maeneo mbalimbali wanayotoka.

Rais wa Chama cha Maofisa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Codepato), Sunday Wambura, alisema chama hicho kitatekeleza maagizo yaliyotolewa na viongozi lengo ikiwa ni kuhamasisha maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini.

Wambura alisema baada ya kuzinduliwa kwa chama hicho, watahakikisha wanafanya kazi zao kwa kujiamini na kufuata sera na miongozo inayowataka kufanywa.



Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna (kulia), akikagua vibanda vya wafanyabiashara ndogondogo maarufu wamachinga jana, vinavyotakiwa kuwapo ni vya kuhamishika kwa ajili ya kuliweka jiji hilo katika mazingira ya usafi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Huduma za upasuaji zaimarika Mundemu

**Na Renatha Msungu,** BAHI

KUTOKANA na kuimarika kwa huduma za upasuaji, Kituo cha Afya Mundeme, wilayani Bahi, kitakuwa na uwezo wa kuwafanyia huduma hiyo wajawazito kati ya 50 hadi 70 kwa mwezi.

Kukamilika kwa huduma hiyo kumelifanya Shirika lisilo la serikali la World Vision kutoa msaada wa vifaa tiba katika kituo hicho, vyenye thamani ya Sh. milioni 16 ili kutoa huduma bora kwa wananchi. Akizungumza jana wakati wa kukabidhi vifaa hivyo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Dk. Filipina Filipo, alisema msaada huo umefanikisha wilaya hiyo kuwa na vituo vya afya vitatu vinavyotoa huduma ya upasuaji na kuondokana na changamoto ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma.

Dk. Filipo alisema kituo cha Mundemu pekee kinahudumia zaidi ya watu 50,000 wa tarafa ya Mundemu na zingine za jirani, hivyo wakazi wa tarafa hiyo watapata huduma za upasuaji katika eneo lao kwa gharama nafuu.

Alisema kituo hicho cha afya kitapunguza vifo vya wajawazito na watoto na mafanikio yameanza kuonekana kwa kuwa mwaka jana kulikuwa na vifo viwili.

"Hii itasaidia kupunguza vifo vya wajawazito kutoka 44 kati ya vizazi hai 100,000 hadi kufikia vifo 22, " alisema.

Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. Anthony Mhimbira, alisema vifaa hivyo vitasaidia katika huduma ya upasuaji kwa kuwa wajawazito wengi walikuwa wanapewa rufani kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kutokana na kutokuwa na vifaa vya kutosha.

Alisema kituo hicho kilikuwa na uwezo wa kufanyia upasuaji wanawake watatu kwa siku kutokana na kutokuwa na vifaa lakini kwa sasa watawafanyia kinamama 10 kwa siku.

Naye Meneja wa Mradi wa Afya ya Mama na Mtoto kutoka shirika hilo, Daudi Gambo, alisema vifaa walivyotoa ni pamoja na kile cha kupima afya ya mgonjwa wakati wa upasuaji na kufuatilia mapigo yake ya moyo.

Vingine ni mizani kwa ajili ya kuwapimia watoto wachanga, kifaa cha kuchemshia vifaa baada ya kutumika, mzani kwa ajili ya kupima urefu na uzito kwa wajawazito.

Aidha, alisema wametoa kifaa cha kupimia mapigo ya mtoto tumboni ili kupunguza malalamiko ya kinamama kwa madaktari kuwa watoto wao walikuwa wanacheza.

# Waonywa kufanya biashara mitaroni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewaonya wafanyabiashara wadogo kuacha tabia ya kufanya biashara kwenye mifereji ya maji kwa kuwa wanachafua mazingira na kuhatarisha afya za walaji.

Onyo hilo alilitoa jana alipokuwa akikagua maeneo wanayofanyia biashara ili kuhakikisha jiji hilo linakuwa safi.

Alisema kufanya biashara kwenye mifereji kutasababisha kuziba kwa mifereji hiyo msimu wa mvua na kuchangia maji machafu kushindwa kupita.

"Sehemu ambazo si rafiki kwa kufanya biashara zenu ni kwenye mifereji inayopitisha maji na kandokando ya barabara na watembea kwa miguu," alisema.

Aliwataka wafanyabiashara kufuata maelekezo yaliyotolewa na Halmashauri ya Jiji ili kufanya biashara zao kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo.

"Rais wetu kwa kushirikiana na halmashauri za majiji na manispaa zote, amewapa wafanyabiashara heshima kubwa ya kufanya shughuli zao kwa uhuru. Kinachotakiwa kwenu ninyi ni kutii na kuzingatia maagizo na kufuata kanuni na sheria," alisema.

"Wafanyabiashara mnatakiwa kuthamini na kuheshimu fursa hii kwa kutofanya kwenye maeneo yasiyo rasmi kupanga biashara," aliongeza.

Aidha, amewataka wamachinga hao kutengeneza matolori ambayo watatumia kufanya biashara kwa urahisi badala ya kuacha meza zao zikizagaa barabarani.

Alisema jiji hilo limetoa baadhi ya maeneo ya barabara kufanyika biashara nyakati za jioni hivyo ni vyema wakatumia matolori ili kurahisisha kuhama badala ya kuacha meza zikizagaa.



# Waziri aagiza shule iwe na walimu 'spesho'

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar , Riziki Pembe Juma, ameitaka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya Serikali, kupeleka walimu mahiri kwenye Shule ya Mambo Sasa.

Alitaka kuhakikisha kuwa walimu watakaopelekwa kufundisha katika shule ya Mambo Sasa wanakuwa na uwezo ili kufikia malengo ya kujengwa shule hiyo.

Shule Msingi Mambo Sasa imejengwa na Jamhuri ya China.

Alisema Mambo Sasa mpya imejengwa kitaalamu zaidi kwani kuna miundombinu ya kisasa ya kufundisha ikiwamo maabara za sayansi na madarasa ya kompyuta.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya Shule mpya ya Msingi Mambo Sasa, katika ukumbi wa Wizara ya Elimu Mazizini Mjini Unguja, Riziki alisema ni vyema kuthamini mchango waliotoa ili kuwatia moyo wadau wa maendeleo waweze kuwa na imani ya kufadhili zaidi sekta ya elimu.

Alisema kuwapo walimu wenye uwezo pamoja na mazingira mazuri ya kusoma na kusomesha kutasaidia kutoa matokeo bora ikiwamo kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi katika shule hiyo na hata kufikia malengo ya kujengwa kwake.

Aidha, Waziri wa Elimu aliwaomba watendaji wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali, kuwa na ushirikiano na watendaji wa wizara hiyo ili kufikia malengo ya kuboresha elimu nchini katika ngazi zote.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Idara Maalum Vikosi vya Serikali, Haji Omar Kheir, alisema ipo haja kwa watendaji wa wizara zote mbili kushirikiana na kupeana taaluma zaidi ili kuondoa changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika kufikia malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kupeleka kila huduma karibu na makazi ya wananchi.

Alisema ugatuzi hauondoi tafsiri ya uwajibikaji kwa walimu na watendaji wengine, bali kilichobadilika ni sehemu ya kupeleka taarifa zao ili kufanyiwa kazi kwa haraka zaidi na kwa wakati.

# Serikali yaomba wadau kuunga mkono viwanda

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI imewaomba wawekezaji binafsi wa viwanda pamoja na wadau wa maendeleo kuipa ushirikiano katika kutekeleza Sera ya Viwanda ya mwaka 2019 - 2029, ili taifa lifikie lengo la kuwa na Zanzibar ya Viwanda.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alitoa ombi hilo wakati wa hafla ya uzinduzi wa vitabu vitano vya Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar iliyofanyika Kikwajuni mjini hapa. Alisema Sera ya Viwanda ikiwa ni miongoni mwa vitabu vilivyozinduliwa na kupata baraka zote za serikali, inatarajiwa kuchangia kuimarisha kwa sekta hiyo hasa kwa kuzingatia kwamba wakati wa utayarishaji wake imewashirikisha wadau walio wengi. Alisema maoni na michango ya wadau yamezingatiwa. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alisema sera hiyo ni matokeo ya mapitio ya sera ya viwanda ya mwaka 1998 iliyokuwa imepitwa na wakati ambayo pia inakwenda sambamba na ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 ibara ya 84 (d), inayozungumzia kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara.

"Ninatambua kwamba ili kuitekeleza sera ya viwanda ni lazima kila mshirika apate fursa ya kusoma vitabu hivyo na kwa nafasi yake atimize wajibu ipasavyo," alisisitiza Balozi Seif.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alieleza kwamba kwa vile Sera ya Viwanda Zanzibar imeshapata baraka zote na kukubalika katika ngazi ya juu, Serikali Kuu itajitahidi kuyatekeleza na kuyasimamia yale yote yanayohusu upande wa sekta ya umma.

Nao kwa upande wao wakiwasilisha salamu kwa taasisi zao, Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa Linalosimamia Viwanda (UNIDO), Stephen na Mwakilishi wa Balozi wa Sweden, nchini Jane Akebak, walisema mafanikio makubwa ya uimarishaji wa sekta ya viwanda utafanikiwa, endapo sera hiyo itaimarishwa na kuwa wazi.

Walieleza kwamba UNIDO, pamoja na washirika wengine wataendelea kuiunga mkono Zanzibar katika mikakati ya kuifanya kuwa taifa la viwanda.

Akimkaribisha mgeni rasmi kuzindua vitabu hivyo Waziri wa Biashara na Viwanda Balozi Amina Salum Ali, alisema uzinduzi wake umetoa mwanga kwa safari ya Zanzibar kuelekea kwenye maendeleo ya uhakika.

Balozi Amina alisema Wizara ya Biashara itaendelea kubeba dhima ya kuiona Zanzibar inastawi na kufanikiwa katika biashara inayotoa fursa katika utoaji wa ajira miongoni mwa wananchi walio wengi.

Vitabu vitano vilivyozinduliwa ni pamoja na Sera ya Viwanda, Ripoti ya Tathmini ya Mazingira ya Ufanyaji wa Biashara, Daftari la Wafanyabiashara, Mwongozo wa Usafirishaji na Uagizaji pamoja na Taarifa za Wazalishaji wa Kazi za Mikono Zanzibar vinavyotarajiwa kuuzwa kwa wateja mbalimbali.



Mwendesha guta akipita kwa tabu kwenye matope kutokana na barabara kuharibika katika eneo la njia panda ya Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# UWT yataka ushindi 2020

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Mkoa wa Magharibi Zainabu, Ali Maulid, ameagiza uongozi wa ngazi za matawi hadi wilaya mkoani humo, kuandaa mipango mikakati ya kufanikisha ushindi wa CCM, 2020.

Alisisitiza kuwa ushindi huo ni lazima upatikane katika uchaguzi mkuu wa dola mwaka 2020.

Agizo hilo alilitoa katika ziara maalumu ya Kamati ya Utekelezaji ya UWT ya Mkoa ya kutembelea majimbo 13 ya umoja huo, katika Jimbo la Dimani Unguja.

Alisema huu ni wakati wa kazi, hivyo kila mwanachama anatakiwa kutumia uwezo na maarifa yake kuhakikisha CCM inashinda.

Zainabu, alifafanua kuwa mipango mikakati hiyo baada ya kuandaliwa ni lazima itekelezwe kwa vitendo ili kuongeza tija katika mikakati na kujiimarisha kisiasa kuelekea uchaguzi mkuu ujao.

Katika maelezo yake mwenyekiti huyo alisema ziara hiyo itafanyika kwa kuzuru majimbo yote ya mkoa huo na kusikiliza changamoto na ushauri wa viongozi, watendaji na wanachama wa ngazi mbali mbali kisha kutoa maelekezi yatakayosaidia utatuzi wa changamoto hizo.

"Ziara hii ni ya kikazi zaidi kwani hakuna muda tena wa kusema tu bila kutenda. Ni lazima kinamama wenzangu tuwe mstari wa mbele kulinda heshima ya historia yetu ndani na nje ya CCM kwani sisi ni jeshi kubwa la kufanikisha ushindi wa chama.", alisema.

Mjumbe wa Kamati ya UWT, Fatma Ali Ameir, akizungumza katika ziara hiyo aliwasihi kinamama hao kuepuka kufanya kampeni za kuwanadi watu wenye nia ya kugombea uongozi kabla ya wakati uliopangwa kisheria.

"Viongozi bado wapo madarakani halafu wanajitokeza wengine wanataka kuchukua nafasi zao, hiyo si tabia njema kwani inaweza kuleta machafuko ndani ya Chama Cha Mapinduzi," alionya Fatma.

Alisema ni muhimu kila viongozi na wanachama ndani ya UWT wafuate miongozo, kanuni na maelekezo ya katiba za umoja huo na Chama Cha Mapinduzi ili kujiepusha na migogoro.

# Waziri ataka makubaliano ya uendeshaji bustani wanyama

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tawa) kukutana na uongozi wa mkoa wa Tabora mara moja ili kujadili namna ya kuifufua upya Bustani ya Wanyamapori Hai ya Tabora (Tabora Zoo).

Pia ameigiza Tawa kuingia mkataba wa makubaliano wa namna ya kuiendesha bustani hiyo badala ya kuendelea kuvutana ilhali wote ni serikali moja.

Kanyasu alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara katika bustani hiyo kutokana na fuatia malalamiko kutoka kwa wabunge wa mkoa wa Tabora kwa madai kuwa bustani hiyo imetelekezwa.

Alisema majadiliano kuhusu namna ya kuiendesha bustani hayo kati ya mkoa na Tawa yalianza tangu mwaka 2012 lakini hadi sasa hayajafikia mwafaka

Kutokana na hali hiyo, alisema haoni sababu za msingi ya suala hilo kuchukua muda mrefu kama Tawa inataka tu kuiendesha bustani hiyo na si kutaka umiliki wa moja kwa moja yakiwamo majengo na eneo la bustani.

"Sisi ni serikali moja, fikieni mwafaka wa namna ya kuiendesha bustani hiyo kwa ajili ya manufaa ya taifa," alisisitiza Kanyasu.

Alisema kushindwa kufikia mwafaka baina ya pande hizo mbili kunawanyima fursa wakazi wa Tabora na mikoa ya jirani kufurahia uwapo ya bustani hiyo katikati ya mji huo wa kihistoria.

Akizungumzia utalii kupitia bustani hiyo, Kanyasu alisema takriban asilimia 98 ya wanyamapori nchini wako katika hifadhi, hivyo kufufuliwa kwa bustani hiyo kutatoa mwanya kwa watu wengi kufanya utalii wa ndani kwa gharama nafuu zaidi.

Kutokana na hali hiyo, Kanyasu alitaka makubaliano hayo yafanyike haraka iwezekanavyo ili Tawa iongeze wanyamapori katika eneo hilo pamoja kukarabati baadhi ya mabanda ambayo yamechakaa kwa kiasi kikubwa sasa.

Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora, Amos Nyenda, amesema mkoa huo uko tayari kuona bustani hiyo inasimamiwa na Tawa lakini kumekuwa na mawasiliano hafifu baina ya pande hizo mbili.

Alisema kuimarika kwa bustani hiyo kutachochea utalii wa ndani kwa vile wananchi baada ya kutembelea bustani hiyo watatamani kutembelea hifadhi ili wakajionee wanyamapori ambao hawamo kwenye uzio.



Mshtakiwa Mchungaji Henry Ozoemana Ogwuanyi (wa pili kulia), akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza baada ya kesi inayomkabili ya kupatikana na dawa za kulevya aina ya Heroin kuahirishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MCT yakemea uandishi unaochochea chuki

**Na Enock Charles**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limekemea vikali mwenendo wa baadhi ya vyombo vya habari vya kimapokeo na vya mtandaoni kutoa taarifa zenye mwelekeo wa kuchochea chuki, uongo na zenye lugha ya kuudhi ili kuendelea kudumisha amani na utulivu nchini.

Katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na baraza hilo na Katibu Mtendaji, Kajubi Mukajanga, imevikumbusha vyombo vya habari kuzingatia maadili katika kutoa taarifa zenye kauli za viongozi kama vile viongozi wa kisiasa na kidini, huku akivionya vyombo hivyo kutotumika kwa maslahi binafsi bali kwa maslahi ya umma.

"Kumeibuka vyombo vya habari vinavyoitwa vya kimkakati ambavyo vimejikita katika kuandaa na kusambaza taarifa zinazochochea chuki, vikitumia lugha za matusi na zisizo na staha kinyume na utamaduni wa Mtanzania na matakwa ya taaluma," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Baraza hilo limeonya kutolewa kwa taarifa za uongo na kupaka watu matope na kuvitaka vyombo hivyo kuzingatia taaluma na maadili yanayovitaka kuthibiti madhara katika habari kabla ya kumfikia msomaji, likitahadharisha kuibuka kwa uhasama baina ya viongozi na wananchi iwapo taarifa hazitathibitishwa kufuata misingi ya taaluma.

Aidha, kuelekea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani vyombo vya habari vimetakiwa kutotumika kama vipasa sauti vya kuchochea chuki na uhasama katika jamii kwa kusambaza uzushi, matusi, vitisho na chuki.

# Mil. 100/- kujenga nyumba za walimu

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imetoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nne za walimu wa Shule ya Sekondari mpya ya Kata ya Tegeruka, iliopo Wilaya ya Musoma mkoani Mara.

Wakati serikali ikitoa kiasi hicho cha fedha, wakazi wa Kata ya Tegeruka, yenye vijiji vya Kataryo, Mayani na Tegeruka wanachangia nguvukazi kwenye ujenzi huo kwa kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vicent Anney, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu na kusema, nyumba mbili zimeshaezekwa bado kupiga lipu na sakafu.

"Nyumba nyingine mbili ziko katika hatua ya mwisho kukamilika kwani mafundi wameshamimina zege la renta, huku vyoo vya shule navyo vikiendelea kujengwa," alisema Dk. Anney.

Kwa upande wake Mkuu wa Shule ya Sekondari Tegeruka, Anthony James, alisema sekondari yake ina uhitaji wa nyumba 17 za walimu, lakini kwa sasa zipo tatu, hivyo ina upungufu wa nyumba 14.

"Hivyo kukamilika kwa nyumba mpya nne zinazojengwa, kutasaidia kupunguza changamoto kwa baadhi ya walimu wa sekondari yetu wanaofundisha na kuishi mbali na shule," alisema James.

Mwalimu huyo alisema wananchi na viongozi mbalimbali wamekuwa mstari wa mbele kuchangia shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao kama ambavyo na sasa wamejitolea nguvukazi zao katika ujenzi wa nyumba hizo.

"Kinachofanywa na wakazi wa Kata ya Tegeruka kinaonyesha ni jinsi gani wanavyounga mkono juhudi za serikali za kuondoa kero mbalimbali kwenye sekta ya elimu," alisema.

Aidha, mkuu huyo wa shule alisema, Tegeruka ina upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi, kwa vile Fizikia yupo mmoja, Baiolojia mmoja, Kemia wawili na Hisabati wawili.

"Shule yetu ina walimu watatu wa kujitolea wa masomo ya sayansi, ambao wanalipwa posho na wazazi wenye wanafunzi na bado kuna upungufu wa walimu wa Kiingereza, Jiografia na Hisabati," alisema.

Alifafanua kuwa shule yake ilishapokea vitabu vya kutosha vya masomo ya sayansi kutoka kwa Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, lakini anamwomba awasaidie kupata walimu wengine zaidi wa kujitolea.

"Tunamwomba pia mbunge aje Desemba mwaka huu kwa ajili ya kufanya harambee kwa ajili ya ujenzi wa maabara tatu za masomo ya sayansi," alisema.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MCHANGANYIKO

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport.
Call: +255 754 375 967.
Email: gold@goldtz.net

## VIWANJA / MASHAMBA


**SHAMBA LINAUZWA**

Shamba la Ekari 13 linauzwa liko Mlandizi barabara iendayo Bagamoyo, lina miti ya matunda inayozaa, lina umeme. Lina maji ya DAWASCO na maji ni matamu. Pia kuna kisima kirefu. Kwa mawasiliano piga simu namba 0655 099825 / 0767 237404 / 0715 237404.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA


## PASSPORT IMEPOTEA



Bw. FERDINAND. F.NACHENGA AMEPOTELEWA NA PASSPORT (HATI YA KUSAFIRIA)

**TAARIFA MUHIMU:**

1. NAMBA YA PASSPORT NI AB.498324
2. TAREHE YA KUZALIWA 01.MAY.1987
3. MAHALI ALIPOZALIWA KILOMBERO
4. TAREHE YA KUTOLEWA 30.NOV.2011
5. MAHALI ILPOTOLEWA DAR-ES-SALAAM
6. MWISHO WA MATUMIZI 29.NOV.2021

**YEYOTE MWENYE TAARIFA APELEKE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI NI KUMB No.NJ/RB/4811/2019. CONTROL NUMBER 991081010 3024.**

115478102

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Mary Audax Rutta anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari. Aina ya gari ni IST nyeusi yenye namba za usajili T 420 CLE. Chassis No. NCP610082738 mwaka huu. yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
KW/RB/1018/2019.

115477002

## KADI YA GARI IMEUNGUA

CHOICE MOTORS LTD anatangaza kuungua kwa kadi ya gari iliyosajiliwa kwa namba T595BCR
Chassis No GX1006126022,
Engine No IGFE6679168
TOYOTA CRESTA.

Tukio limeripotiwa kituo cha polisi 09/04/2019 na GIFT D KOWERO.

ARU/ARU/RB/408797/2019.


115477302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AREEQ AMRAN MOHAMED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 994 DKW TOYOTA BREVIS.** Chassis No. **JCG100042565.** Engine No. **1JZ1140879.** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituoa cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/RB/1370/2019.**

115477902

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMMY ALOYCE ALOYCE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4860/0008 kilichotolewa na **SEKONDARI YA ST. THOMAS NYABULA IRINGA** mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi: DAR/CHA/RB/409172/2019.**

115477601


Uza,
Chenye Thamani
Kubwa Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0767 223311


## TREKTA LINAUZWA

GURU ENGINEERING WORKS LTD inauza Trekta aina ya SONALIKA INTERNATIONAL HP 75 ZERO KLM.

Kwa mawasiliano piga simu namba **0712 233333.**

115476902

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO….. OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late NOEL MICHAEL MASAKA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ISAKA MICHAEL MASAKA.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.


Objections to the grant should be filled on or before the 30 Day of October, 2019.

Dated at Dodoma this 2ND day of October, 2019.

…………………………………………………….
PETITIONER
Presente

115477402

## KUPOTEA KWA CHETI



**LEIYABU MAGOMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1402/0055 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari KASAMWA.

Yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **NZ/RB/4800/2019**

115477102


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

TANGAZO

BancABC part of atlasmara

# TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Jun-19 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,521 | 3,705 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12,015 | 7,367 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 33,025 | 32,774 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,548 | 4,452 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | (48) | 190 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 91,839 | 94,037 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 130,381 | 132,226 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 33,902 | 34,172 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 4,109 | 4,391 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **315,291** | **314,314** |
| B | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 91,364 | 97,633 |
| 18 | Amana za Wateja | 97,865 | 89,299 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 25 | 50 |
| 27 | Dhima Nyingine | 5,869 | 6,303 |
| 28 | Madeni | 68,364 | 67,881 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **263,487** | **261,165** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **51,804** | **53,149** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 116,014 | 116,014 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | 1,284 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (61,839) | (63,123) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (3,433) | (2,091) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,062 | 1,065 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **51,804** | **53,149** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 7,711 | 8,130 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 21,077 | 22,303 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 16,060 | 19,807 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16.4% | 16.9% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 14.4% | 14.8% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 77.4% | 81.3% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 41.4% | 42.1% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 82.7% | 83.8% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1.2% | -3.5% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.3% | -0.8% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-19 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Sep-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,859 | 11,825 | 32,045 | 39,116 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,699) | (5,074) | (14,152) | (17,214) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **6,160** | **6,751** | **17,894** | **21,902** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa/ Yaliorejeshwa | 566 | - | 1,663 | (8,327) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (700) | (1,434) | (2,154) | 596 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,380** | **1,707** | **3,997** | **4,221** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 434 | 718 | 1,432 | 1,439 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 814 | 300 | 2,191 | 799 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 132 | 689 | 374 | 1,983 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(8,704)** | **(8,232)** | **(24,695)** | **(23,495)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,750) | (2,454) | (8,077) | (7,567) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (5,953) | (5,778) | (16,618) | (15,928) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,297)** | **(1,208)** | **(3,297)** | **(5,103)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (45) | - | (136) | (48) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,342)** | **(1,208)** | **(3,433)** | **(5,151)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,342)** | **(1,208)** | **(3,433)** | **(5,151)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 156 | 156 | 156 | 156 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.55) | (0.49) | (0.35) | (0.52) |
| 15 | | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 7 | 7 | 7 | 7 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.71% | -1.42% | -1.45% | -3.02% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -10.23% | -8.45% | -8.72% | -18.02% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 115.43% | 97.33% | 112.81% | 89.94% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.64% | 2.95% | 3.53% | 4.79% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2019(Kiasi kwa shilingi milioni

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-19 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-19 |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,297) | (790) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 1,588 | 1,560 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1,054 | 1,463 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2,297 | (6,807) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - 250 | 1,801 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (459) | 2,522 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 507 | (923) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (45) | - |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za** | **3,395** | **(1,173)** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (35) | (163) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za** | **(35)** | **(163)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | 2,738 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **2,738** |
| | | - | - |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 3,361 | 1,401 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 109,562 | 108,161 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **112,923** | **109,562** |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2018

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **116,014** | **-** | **(67,756)** | **-** | **1,284** | **1,065** | **50,607** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (3,433) | - | - | - | **(3,433)** |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1,284 | - | (1,284) | - | - |
| Mengineyo | - | - | 4,633 | - | - | (3) | **4,630** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **116,014** | **-** | **(65,272)** | **-** | **0** | **1,062** | **51,804** |
| | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **116,014** | **-** | **(69,349)** | **9,118.58** | **1,114** | **1,384** | **58,282** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (7,355) | - | - | - | **(7,355)** |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 9,118 | (9,118) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (170) | - | 170 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (320) | **(320)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **116,014** | **-** | **(67,756)** | **0** | **1,284** | **1,065** | **50,607** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 25-Oct-19 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 25-Oct-19 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 25-Oct-19 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | Dr J P. Kipokola | | 25-Oct-19 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 25-Oct-19 |

215478302

BancABC
part of
atlasmara

# MINIMUM DISCLUSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | Free | Free | Free |
| | | | |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| | | | |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| | | | |
| CURRENT ACCOUNT | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 2,000.00 | N/A | N/A |
| | | | |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 2,000,000.00 | $ 2,000.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 5,000.00 | $ 10.00 | N/A |
| | | | |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 3,000,000.00 | $ 3,000.00 | £ 3,000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| | | | |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | £ 1,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | £ 5,000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |

| GENERAL CHARGES | | | |
|---|---|---|---|
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| | | | |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 120.00 | N/A |
| Technical | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | N/A |
| | | | |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 30,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| 100 leaves | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | £ 60.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 10% Per Cheque | 10% Per Cheque |
| **Stop Payment Charges** | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | £ 50.00 |
| | | | |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | TZS 10,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | TZS 4,000.00 | $ 3.00 | £ 2.00 |
| Standing Order - Other local bank | TZS 40,000.00 | $ 30.00 | £ 20.00 |
| Amendment | TZS 5,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| | | | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| - Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| - Cash Deposit at Branch small denominations 500 above 50( | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch small denominations (2,000 and be | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 0.3% Min 1,000 | N/A | N/A |
| With Account Transfers (Internal) | N/A | N/A | N/A |
| - Cheque deposit | Free | Free | Free |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to | TZS 2,500.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 5 | TZS 6,000.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) abov | 0.15% MAX 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3000 Max 200000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 7,500 Max 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| - Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 2%On small denominations* | 2%On small denominations* |
| | | | |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account monthly fee | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 5,000.00 | $ 3.00 | £ 3.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Reference Letter | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | Comm 0.25% Min 50 Max 500 | comm 0.25% min 50 max 350 |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% per qtr min $200 | 1% per qtr min $200 |

215478302

# FLAMENGO KUIVAA RIVER PLATE FAINALI COPA LIBERTADORES




**RIO DE JANEIRO,** Brazil

KLABU ya Brazil ya Flamengo iliibuka na ushindi mnono wa mabao 5-0 dhidi ya Gremio 5-0 juzi, Jumamosi na hivyo kufuzu kucheza fainali ya Kombe la Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini, Copa Libertadores.

Flamengo itacheza na River Plate ya Argentina kwenye fainali ya michuano hiyo yenye hadhi sawa na ile ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Klabu hiyo yenye maskani yake jijini Rio de Janeiro ilianza kufunga bao lake kupitia kwa Bruno Henrique (pichani) kwenye mchezo huo uliopigwa katika dimba la Maracana dakika ya 42.

Lakini mchezo huo uliohudhuriwa na mashabiki 70,000 ulikuwa na burudani zaidi katika kipindi cha pili.

Gabriel Barbosa akafunga bao la pili dakika ya 46 na la tatu dakika ya 56, huku Pablo Mari akiongoza la nne dakika ya 67 na Rodrigo Caio akafunga la tano dakika ya 70.

"Tumeandika majina kwenye historia ya Flamengo," alisema Gabriel Barbosa, ambaye ndiye alikuwa nyota wa mchezo huo na mabao yake hayo mawili yalimfanya kuwa kinara wa mabao kwenye michuano hiyo ya Libertadores.

"Kwa uhakika kuna mchezo mmoja unakuja, lakini tunafuraha kwamba tumeingia fainali."

Katika mchezo wa kwanza uliopigwa kule Porto Alegre mwanzoni mwa Oktoba ulimalizika kwa sare ya kufungana bao 1-1 na hivyo, ushindi sasa wameshinda kwa uwiano wa mabao 6-1.

Flamengo, ambayo pia inaongoza kwenye msimamo wa Ligi ya Brazil, kwa mara ya mwisho ilishinda taji hilo mwaka 1981, wakati nyota wa zamani wa Brazil, Zico, Junior na Leandro walipokuwa wanaichezea timu hiyo.

# Conte: Dortmund hofu tele Inter

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amedai kwamba, Borussia Dortmund waliihofia Inter Milan, baada ya Nerazzurri hao kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi yao kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, Jumatano.

Lautaro Martinez na Antonio Candreva kila mmoja alifunga bao moja kuiwezesha Inter kupata ushindi huo kwenye dimba la San Siro, ambapo Waitaliano hao walipata ushindi wao wa kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya chini ya Conte.

Martinez, ambaye penalti yake ya kipindi cha kwanza iliokolewa – ameiifungia mabao matano Inter katika mechi nne zilizopita, alianza kufunga dakika ya 22 kabla ya Candreva kufunga la pili ikiwa imebakia dakika moja mpira kumalizika.

Ulikuwa ni ushindi wa kwanza kwa Inter dhidi ya timu kutoka Ujerumani tangu Machi mwaka 2011 na kocha Conte mara baada ya mchezo huo aliiambia Sky Sport Italia: "Borussia Dortmund walibadilisha mfumo wao mara tano nyuma, kitu ambacho kinaonyesha walituhofia.

"Tulijiandaa kwa mchezo tofauti, lakini tulifanya vizuri, wakati Dortmund walipobadilisha mfumo wa 4-2-3-1 baada ya mapumziko, na sisi tukabadilika na kutawala mchezo. "Tulijiandaa kucheza mpira kwa nguvu na kubadilisha mfumo wetu, hivyo tukaweza kuwatawala kirahisi.

"Kitu muhimu niliwaambia wachezaji wangu kwamba, tubadili mfumo kwa kuhakikisha kwamba, tunasukumiza mashambulizi mbele na kucheza kwa mashambulizi ya kushtukiza."

Inter sasa wana pointi nne kutokana na mechi tatu walizocheza kwenye Kundi F na wamejivuta nafasi ya pili nyuma ya Dortmund wakitofautiana kwa idadi ya mabao na wamepitwa pointi tatu na vinara wa kundi hilo Barcelona.





# *Anayewania Ballon d'Or ajitangaza mjamzito*

**NEW YORK,** Marekani

ALEX Morgan amebainisha kwamba yeye ni mjamzito ikiwa ni miezi mitatu tu tangu alipoisaidia Marekani kushinda Kombe la Dunia kwa Wanawake.

Mshambuliaji huyo wa klabu ya Orlando Pride anatarajia mtoto wake wa kwanza na mume wake, Servando Carrasco, ambaye ni kiungo wa klabu ya Galaxy, Aprili mwaka 2020. Na mtoto huyo ashajulikana jinsia yake kuwa ni wa kike.

Galaxy iliwapongeza wanandoa hao kupitia ukurasa wake wa Twitter, kabla ya Morgan kuweka picha katika ukurasa wake wa Instagram.

"Tumekuwa kwenye mapenzi naye, ingawa bado hatujampokea," aliandika. "Mwanachama mpya katika familia ya Carrasco, anakuja hivi karibuni."

Morgan alifunga mabao sita kwenye Kombe la Dunia na matano akifunga kwenye ushindi wa rekodi ya mabao 13-0 dhidi ya Thailand – na Marekani alikuwa bingwa mtetezi.

Wiki hii alitajwa kwenye tuzo ya mwaka 2019, Ballon d'Or Femenin (Tuzo ya mwanasoka bora wa kike wa mwaka).

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, hajaichezea Orlando tangu alipoumia dakika ya 13 kwenye mchezo wa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Chicago Red mwishoni mwa Agosti.

Morgan alibainisha mwezi uliopita kwamba, kuumia kwake goti kumetamatisha muda wake wa kuichezea ligi ya soka ya Taifa ya Wanawake kwa msimu huu.

## Klopp: Mengi zaidi yaja kwa Oxlade-Chamberlain

**LONDON,** England

JURGEN Klopp anaamini bado kuna mambo mengi zaidi yanakuja kutoka kwa Alex Oxlade-Chamberlain baada ya kiungo huyo kufunga mabao mawili wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa 4-1 dhidi ya Genk kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumatano.

Oxlade-Chamberlain alikuwa nje ya uwanja kwa miezi 18 kabla ya kurudi juzi kucheza kwa kiwango bora katika mchezo huo ambao Liverpool ilikuwa ugenini.

Moja ya mabao alifunga kwa ustadi baada ya kuubetua mpira akiwa nje kidogo ya eneo la hatari.

"Alicheza kwa kiwango cha aina yake, lakini naweza kusema timu nzima ilicheza kwa ustadi," alisema Klopp.

"Naamini kuna mengi zaidi yanakuja kutoka kwake, kwa sababu alikuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu na sasa amerejea uwanjani kwa kiwango cha kuvutia.

"Bado kuna mechi nyingi, hivyo ana nafasi ya kutibitisha ubora wake na sina shaka kwa hilo," alisema Klopp.

Mabao mengine ya Liverpool yalifungwa na washambuliaji Sadio Mane na Mo Salah.

Liverpool ipo nafasi ya pili katika Kundi E ikiwa na pointi sita nyuma ya Napoli yenye ponti saba ambayo iliichapa RB Salzburg mabao 3-2.







## MERTENS AVUNJA REKODI YA MARADONA

**NAPLES,** Italia

KOCHA wa Napoli, Carlo Ancelotti amemsifia Dries Mertens aliyevunja rekodi ya mabao ya Diego Maradona kwa kiwango bora zaidi wakati miamba hao wa Italia wakiibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Salzburg kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano.

Mertens aliiweka Napoli mbele mara mbili kabla ya Lorenzo Insigne kutokea benchi na kufunga bao la ushindi kwa vijana hao wa Ancelotti waliopo Kundi E.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, Mertens sasa amefunga mabao 116 kwa Napoli, akishika nafasi ya pili nyuma ya nahodha wa zamani wa kikosi hicho, Marek Hamsik (121).

Mabao hayo mawili ya Mertens yalivunja rekodi ya gwiji wa Napoli, Maradona katika orodha ya wafungaji wa wakati wote wa klabu hiyo ambayo sasa inaongoza kundi lake la E kwa pointi moja dhidi ya bingwa mtetezi wa michuano hiyo, Liverpool.

"Ulikuwa ni usiku mkubwa kwake yeye na kwetu sisi," alisema Ancelotti akiiambia Sky Sports Italia.

"Tulipigana kwa juhudi. Ulikuwa mchezo wa kuvutia na tuliendelea kupambana kwa dakika 90 ni matokeo mazuri kwa upande wetu.

"Tulianza kwa kupambana zaidi, tuliongoza na tulikuwa na wakati mgumu, lakini tulijitahidi na kuweza kutawala mchezo.

## *Lampard: Uvumilivu umelipa kwa Batshuayi*

**LONDON,** England

FRANK Lampard anaamini Michy Batshuayi amepata zawadi yake kwa uvumulivu aliouonyesha msimu huu, baada ya juzi, Jumatano kufunga bao pekee wakati Chelsea ikishinda 1-0 dhidi ya Ajax kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Bao la Batshuayi alilofunga dakika nne kabla ya mpira kumalizika, liliwafanya vijana hao wa pale Stamford Bridge kuondoka na ushindi huo muhimu.

Licha ya kuingia dakika ya 71 akitokea benchi, Batshuayi mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji aliongoza kwa kupiga mashuti manne yaliyolenga lango la Ajax likiwamo lililozaa bao kuliko mchezaji mwingine.

Batshuayi alichukua nafasi ya mshambuliaji chaguo la kwanza wa Lampard, Tammy Abraham, ambaye alikosa nafasi kadhaa za kuipa ushindi Chelsea.

"Kiukweli Christian Pulisic aliingia katika mechi mbili zilizopita na alitengeneza pasi za mwisho mbili na alibadilisha mchezo, ingawa kiwango chake kilidumu kwa dakika 25 tu," alisema Lampard na kuongeza:

"Na Michy ni mshambuliaji wa daraja la juu, nalijua hilo, ingawa Tammy amekuwa akifungwa kwenye timu yangu, hawa wawili walitulia, walijifua kwa bidii, walitoa sapoti kwa timu na wameonyesha kile wanachoweza kukifanya.

"Hivyo, lilikuwa ni chaguo langu kumwingiza Michy, kwa sababu alivyoweza kuonyesha utulivu na uvumilimu."

Chelsea sasa imeshinda mechi mfululizo za ugenini kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2013 na ikiwa inalingana na Ajax kwa kujikusanyia pointi sita baada ya mechi tatu.



DONDO … OKA
MAGAZE … AYA




# MESSI AWEKA REKODI UEFA AKIMFIKIA CR7

**●●● Ni moja ya kushangaza zaidi kwa Leo, ni rahisi kusema lakini ni vigumu sana kuiweka...**

**PRAGUE,** Czech

LIONEL Messi amekuwa mchezaji wa kwanza kuweza kufunga katika misimu 15 mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Barcelona ikipata ushindi hafifu ugenini dhidi ya Slavia Prague juzi.

**Messi ambaye aliifungia Barcelona bao la kuongoza wakati wakishinda 2-1, mbali na rekodi yake hiyo mpya, ameingia katika kitabu cha rekodi cha Ligi ya Mabingwa na kuwa pamoja na Cristiano Ronaldo na Raul.**

Lilikuwa ni bao rahisi la umaliziaji kwa Messi, 32, baada ya kugongeana vema na Arthur na hivyo kuendeleza makali yake akitokea chumba cha majeruhi na huo ukiwa mwanzo mzuri wa msimu kwake.

Bao hilo pia lilimfanya Messi kuifikia rekodi ya nguli wa Real Madrid, Raul na mpinzani wake, Ronaldo kama wachezaji ambao wamefunga dhidi ya wapinzani 33 tofauti kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akizungumzia rekodi hiyo, Kocha wa Barcelona, Ernesto Valverde alimsifu mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina kwa kuivunja huku akifafanua kwamba sasa anarejea katika ubora wake akitokea chumba cha majeruhi.

Valverde aliwaambia wanahabari baada ya mechi hiyo: "Ni mchezaji ambaye anaweza kuamua katika kila mchezo. Kila siku tunamuona ni bora zaidi.

"Rekodi moja zaidi ya kushangaza kwa Leo. Ni rahisi kusema, inaonekana ya asili, lakini ni vigumu sana kuiweka."

Baada ya Messi kufunga bao hilo, Slavia iliweza kusawazisha kupitia kwa Jan Boril dakika tano baada ya kipindi cha pili kuanza, lakini kimya kingi kilitanda kufuatia Barca kunufaika na bao la kujifunga la Peter Olayinka lililotokana na shuti la Luis Suarez kumbabatiza.

Ushindi huo uliifanya Barca kufikisha pointi saba kutokana na mechi tatu za Kundi F, zikiwa ni tatu zaidi mbele ya Inter na Borussia Dortmund. Kuhusu Messi, Kiungo wa Barca Sergio Busquets aliongeza: "Alikuwa na mwanzo mgumu wa msimu kwa sababu ya majeraha. Yeye ni wa msingi kwa jinsi tunavyocheza na mengi hupitia kwake.

"Anarudisha dansi yake, lakini haitamchukua muda mrefu kwa sababu ndiye bora zaidi duniani."

## ZISIKUPITE

### CITY HAIPOI KWA RUIZ

MANCHESTER City wamepiga hatua ya kumnasa kiungo wa Napoli, Fabian Ruiz na juzi Jumatano walituma mashushushu kwenye mechi yao ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Red Bull Salzburg kumwangalia. ***(Guardian)***

### UPAMECANO AWINDWA ARSENAL

ARSENAL itafanya mabadiliko ya bei kwa beki wa kati wa RB Leipzig, Mfaransa Dayot Upamecano, 20, kuondoa hofu katika safu ya ulinzi ya Unai Emery. ***(Sun)***

### AKE KUREJESHWA CHELSEA

MSAKA vipaji wa Chelsea, Piet de Visser ameishauri klabu hiyo kumsajili kwa mara nyingine beki Mholanzi, Nathan Ake, 24, kutoka Bournemouth. ***(Sky Sports)***

### SOLSKJAER ATAKA VISU VIWILI

MANCHESTER United itatazama uwezekano wa kusajili washambuliaji wawili katika dirisha la usajili la Januari wakati huu kocha Ole Gunnar Solskjaer akihitaji nguvu zaidi. ***(Star)***

### SIMON KUMRITHI COURTOIS

REAL Madrid inamwona kipa wa Athletic Bilbao, Mhispania Unai Simon, 22, kama mbadala sahihi wa Mbelgiji Thibaut Courtois, 27. ***(El Desmarque, via AS)***

### MANDZUKIC, JUVE WAJADILIANA

JUVENTUS ipo katika mazungumzo na Mario Mandzukic kuhusu uwezekano wa kumwacha aondoke katika dirisha la usajili la Januari. Straika huyo Mcroatia mwenye umri wa miaka 33 amekuwa akiwindwa na Manchester United. ***(Mirror)***

### RODGERS AMTULIZA MADDISON

BRENDAN Rodgers amemwambia kiungo James Maddison kuwa Leicester ni sehemu sahihi kwake ya "kung'ara" huku kukiwa na kuvutiwa kwa Manchester United kwa nyota huyo Muingereza mwenye umri wa miaka 22. ***(Leicester Mercury)***

### SOLSKJAER AMTAJA KANE

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amemwelezea mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane, 26, kama mmoja wa washambuliaji wenye thamani duniani lakini akakiri hawawezi kumpandia dau. ***(Evening Standard)***

### IBRAHIMOVIC ANUKIA NAPOLI

RAIS wa Napoli, Aurelio de Laurentiis amesema anavutiwa kumsajili Zlatan Ibrahimovic, 38, ambaye atakuwa mchezaji huru dirisha dogo la usajili wakati mkataba wake na LA Galaxy utakapomalizika. ***(ESPN)***

### FABINHO AMTOA DENDA EMERY

UNAI Emery amefunguka kuwa kiungo wa Liverpool, Mbrazil Fabinho, 26, alikuwa windo lake kuu kumsajili wakati alitwaa mikopa ya kuinoa Arsenal mwaka jana. ***(Evening Standard)***

### SPURS YAMFUATILIA SOARES

TOTTENHAM inamfuatilia mshambuliaji wa Gremio, Mbrazil Everton Soares, na mkuu wao wa kuchunguza vipaji, Steve Hitchen hivi karibuni alimtazama nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, kwenye Copa Libertadores. ***(Sky Sports)***

## Kilimanjaro Queens yapangwa na vibonde

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la Chalenji kwa Wanawake, Timu ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens), imepangwa kuanza kutetea taji hilo kwa kuwakaribisha Sudan Kusini, katika mechi ya Kundi A itakayochezwa Novemba 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo ya ufunguzi wa michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya kwanza hapa nchini, itatanguliwa na mchezo kati ya Burundi dhidi ya Zanzibar Queens utakaoanza saa 8:00 mchana kwenye uwanja huo huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), Nicholas Musonye, alisema jumla ya nchi nane zitashiriki mashindano hayo na zimepangwa katika makundi mawili.

Musonye alisema Kundi A litakuwa na wenyeji Kilimanjaro Queens, Zanzibar Queens, Sudan Kusini na Burundi wakati Ethiopia, Kenya, Uganda na Djibouti wako Kundi B ambalo linaonekana kuwa kundi la kifo.

Alisema Kilimanjaro Queens itashuka tena dimba Novemba 16 kucheza dhidi ya Burundi na itakamilisha mechi zake za hatua ya makundi kwa kuwavaa "ndugu " zao, Zanzibar Queens ifikapo Novemba 18, mwaka huu.

## Mkazi wa Mbagala ashinda mil. 100/-

**Na Elizabeth Zaya**

JUMA Kidoga, mkazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam, amejishindia Sh. milioni 100 baada ya kubashiri matokeo kupitia Kampuni ya Michezo ya Kubashiri Matokeo ya Gal ambayo jana ilimkabidhi hundi ya kitita hicho.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa hundi hiyo, Juma alisema amekuwa akicheza mchezo huo wa kubashiri siku nyingi na kubahatisha kujipatia fedha ndogo, lakini sasa ameshinda kitita hicho kinono.

"Nina furaha kubwa kupata fedha nyingi namna hii, kwangu naona ni kama ndoto, nimecheza michezo hii kwa muda mrefu sana, lakini sijawahi kubahatika kama ilivyotokea sasa," alisema

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo ya Gal, Hakan Eric, alisema tangu ianzishwe mwaka 2016, tayari ina wateja zaidi ya milioni 10 dunia nzima.

Mkaguzi wa michezo hiyo kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Bakari Majid, alisema katika michezo hiyo, serikali imekuwa inajipatia kodi.

"Sisi kama serikali tumekuja kujiridhisha kwa sababu katika michezo hii kuna kodi ambayo inapatikana, kwa mfano katika ushindi huu serikali inapata kodi yake zaidi ya Sh. milioni 19," alisema Majid.

# KAGERE AFUNGUKIA BAO LAKE AZAM IKIJIVUNIA KUJITAHIDI

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI Kocha Msaidizi wa Azam FC, Meja mstaafu Abdul Mingange, akisema kwa ubora wa wapinzani wao, vijana wake walijitahidi kupambana kwenye mchezo waliochezea kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Simba Uwanja wa Taifa juzi, mfungaji wa bao hilo pekee, Meddie Kagere amesema haikuwa kazi nyepesi kuweza kuwafunga 'Wanalambalamba' hao.

**Kagere ambaye sasa amefikisha mabao saba kutokana na mechi tano, aliliambia Nipashe kuwa mchezo huo ulikuwa mgumu na wapinzani wao kwa kiasi kikubwa walijitahidi kuwabana na kuwapa wakati mgumu kwa muda mwingi.**

"Nashukuru Mungu tumepata ushindi, lakini haukuwa mchezo mwepesi, Azam ni wazuri na ilitubidi kupambana zaidi kuweza kupata ushindi ambao kila Mwanasimba ameufurahia," alisema Kagere na kuongeza;

"Mabeki wa Azam walicheza vizuri lakini baadaye walionekana kuchoka na kucheza rafu nyingi, kwa sasa tunajipanga kwa ajili ya mchezo unaofuata," alisema Kagere.

Kwa upande wa Mingange, ambaye alishirikiana na Iddi Cheche kwenye benchi la ufundi kuiongoza timu hiyo, kwa kile kinachoonekana huenda mrithi wa Etienne Ndayiragije, Mromania Aristica Cioaba bado hajapata kibali cha kuanza kuinoa Azam FC, alisema pamoja na kufungwa, kwa ujumla vijana wake walijitahidi.

"Simba ni timu nzuri, inawachezaji wazuri, kwa namna walivyocheza na tulivyocheza naamini wachezaji wangu walipambana na kujaribu kuwabana wapinzani wetu licha ya kupoteza mchezo," alisema Mingange.

Aidha, alisema kwa kiasi kikubwa maamuzi kwenye mchezo huo hayakuwa mazuri ingawa alikataa kutoa lawama kwa mwamuzi wa mchezo.

Katika mchezo huo, goli pekee la kipindi cha pili la mshambuliaji Kagere lilitosha kuipa Simba pointi tatu muhimu zinazoifanya kuendelea kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo wakijikusanyia pointi 15 baada ya michezo mitano.

Kikosi hicho cha Simba kinasafiri kwenda Arusha kwa ajili ya mchezo wao unaofuata wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida United wanaotumia kwa muda Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini humo.

Baada ya mchezo huo wa Jumapili, Simba iliyopo kileleni mwa ligi hiyo, itaelekea mikoa ya Kanda ya Ziwa, Mwanza na Shinyanga kabla ya kurejea Dar es Salaam.

NI HIVI...



Kipa wa Taifa Stars, Juma Kaseja (chini), akiwanoa makipa wa Twiga Stars, ambao wanajiandaa na mashindano ya Kombe la Chalenji kwa Wanawake. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Kitimtim Ligi Kuu Zanzibar kuendelea leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KITIMTIM cha mzunguko wa saba wa Ligi Kuu ya Zanzibar unatarajia kuanza kutimua vumbi leo, Ijumaa kwa kupigwa michezo mitatu katika viwanja vitatu kwa Unguja na Kisiwani Pemba.

Katika dimba la Mao A, timu ya Mafunzo ambayo ipo nafasi ya saba ikiwa na alama tisa itavaana na Machomane kutoka Pemba yenye pointi tano katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Uwanja wa Gombani Kisiwani Pemba, timu ya Jamhuri itakuwa mwenyeji wa Chuoni, huku katika Uwanja wa Amaan Mabaharia wa KMKM watavaana na Mwenge ya Kisiwani Pemba.


Akizungungumza na gazeti hili Kocha wa KMKM, Ame Msimu alisema Ligi ya Zanzibar inazidi kuwa ngumu licha ya timu yake kupata matokeo mazuri karibu michezo yote waliocheza.

Alisema hali ilivyo hivi sasa ni vigumu bado kujihakikishia kunyakuwa ubingwa wa Zanzibar kutokana na timu zinazocheza ligi hiyo kujituma ili kuhakikisha hazipotezi mchezo.

"Yaani hata hapo kileleni mwa ligi kama msimamo unavyoonekana leo unaweza kukaa kileleni kesho ukawa nafasi ya pili au ya tatu, ligi yetu licha ya kutokuwa na mdhamini, lakini ni ligi ngumu na hii inatokana na wachezaji wengi kuwa na vipaji vya kucheza soka kwa hiyo ushindani unakuwa mkubwa," alisema.

Timu ya KMKM ambayo ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 16 sawa na Zimamoto ambao ndio vinara wa ligi hiyo.

Michezo
Ijumaa Oktoba 25, 2019
Nipashe



Messi aweka rekodi Uefa akimfikia CR7 UKURASA 30

WAMELIKATAA...



Mtanzania Mbwana Samatta akiruka na kumzidi kimo beki wa Liverpool, James Milner na kuifungia timu yake ya KRC Genk bao la kusawazisha lililokataliwa wakati wakiwa nyuma kwa bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa Uwanja wa Luminus Arena mjini Genk, Ubelgiji na wenyeji kulala kwa mabao 4-1. **PICHA: MTANDAO**

# *Samatta awaamsha wachambuzi England*

## Ni kutokana na bao lake dhidi ya Liverpool kukataliwa, refa wa EPL atoa ufafanuzi huku VAR...

**Genk,** Ubelgiji

HABARI ya mjini barani Ulaya kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa hususan mechi ya KRC Genk dhidi ya Liverpool, si kipigo cha mabao 4-1 walichokipata Wabelgiji hao, bali ni bao la kusawazisha alilolifunga Mtanzania Mbwana Samatta na kukataliwa awali wakati wakiwa nyuma kwa bao 1-0.

**Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Luminus Arena mjini Genk, Ubelgiji na kuchezeshwa na refa Slavko Vincic kutoka Slovenia, ma bao ya Liverpool yalifungwa na Alex Oxlade-Chamberlain aliyetupia mawili kabla ya Sadio Mane na Mohamed Salah kila mmoja kufunga moja.**

Oxlade-Chamberlain alianza kufungua milango ndani ya dakika mbili za mchezo kabla ya Samatta kutupia la kusawazisha dakika ya 26, lakini safari hii VAR ilielezwa kuwa adui mkubwa wa Genk, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Mechi hiyo ililazimika kuchelewa kuendelea kwa dakika mbili kufuatia waamuzi wa Slovakia katika chumba cha VAR kutumia muda huo kutazama kuona kwa nini bao hilo la Samatta aliloruka juu na kuunganisha nyavuni kwa kichwa krosi ya Junya Ito, lilikataliwa na refa, Vincic.

Hata hivyo, refa wa zamani wa Ligi Kuu England, Peter Walton ni miongoni mwa walioamka kuelezea kwa nini bao hilo la Genk dhidi ya Liverpool lilikuwa sahihi kukataliwa kutokana na kuwa la kuotea ['offside'], kuliko kuhisiwa kulitendeka faulo kabla ya Samatta kufunga.

Samatta aliruka juu kuiunganisha krosi ya Ito, na kupiga kichwa cha nguvu kilichomshinda kipa Alisson na kukimbia akishangilia akiamini kuisawazishia miamba hiyo ya Ubelgiji.

Lakini bao hilo lilikataliwa na refa, huku VAR ikilazimika kuchukua muda mrefu kuhakiki usahihi wa kulikataa na kusababisha wengi kuamini Samatta alimchezea madhambi James Milner wakati akiruka kupiga kichwa.

Hata hivyo, refa mstaafu wa EPL, Walton alielezea kwamba mwamuzi Vincic alikuwa ameinua mkono wake wa kushoto mara moja, kuashiria kwamba Ito alikuwa ameotea kabla ya kupiga krosi hiyo iliyomkuta Samatta, hivyo kuwaumiza sana wenyeji.

Bao hilo la Samatta limeamsha wachambuzi wengi wa soka huku ikielezwa Ito alikuwa ameotea kidogo sana kiasi kwamba refa angeweza kupotezea kwa kuwa hata VAR ilipata tabu kung'amua lakini tatizo ni kwamba Vincic alishapuliza kipenga.

Kwa matokeo hayo, yanaifanya Liverpool kushika nafasi ya pili katika Kundi E ikiwa na pointi sita nyuma ya Napoli yenye alama saba ambayo iliichapa RB Salzburg mabao 3-2 juzi.

Genk inaburuza mkia ikiwa na alama moja iliyoipata kwa kutoka sare tasa ilipoialika Napoli.

Majira ya joto yaliyopita, Samatta alihusishwa sana na kutua Ligi Kuu England lakini mchakato huo haukukamilika lakini bado tetesi zinaendelea kumhusisha kwamba msimu ujao huenda akajiunga na moja ya klabu za ligi hiyo pendwa duniani.

Kwa ujumla Samatta jana ilikuwa mechi yake ya 169 kwenye mashindano yote tangu ajiunge na KRC Genk Januari mwaka 2016 akitokea TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) akiwa amefunga mabao 68.

Katika Ligi ya Ubelgiji pekee Samatta amecheza mechi 132 na kufunga mabao 52, kwenye Kombe la Ubelgiji amecheza mechi tisa na kufunga mabao mawili, katika Super Cup mechi moja na Europa League mechi 24 na mabao 14.

## Mo amrudisha Magori, agawa bodaboda Simba

**Na Shufaa Lyimo**

Wachezaji wa Simba na benchi la ufundi wamekabidhiwa zawadi ya pikipiki aina ya Boxer na simu ya mkononi kwa kila mmoja ikiwa ni utekelezaji wa ahadi iliyotolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed "Mo" Dewji baada ya msimu uliopita kutetea ubingwa wa Ligi Kuu na kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hafla ya kukabidhi zawadi hizo ilifanyika jana makao makuu ya Kampuni ya Kuuza Bajaji iliyopo mtaa wa Gerezani Majani ya Chai jijini Dar es Salaam. Akikabidhi pikipiki hizo kwa kila mchezaji, Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya METL, Fatma Dewji alisema hiyo ni ahadi ambayo aliitoa Mo.

"Tumeshukuru sana kuona ahadi ya Mwenyekiti wetu imetimia leo kutoa zawadi ya pikipiki kwa wachezaji," alisema Fatma.

Kwa upande wa Meneja Mkuu wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu alisema amefurahishwa na zawadi aliyoipata na kudai itaongeza chachu ya ushindani ndani ya klabu hiyo.

"Zawadi hizi zimetolewa kwa watu 39 ambao ni wachezaji pamoja na benchi la ufundi lilikokuwa msimu uliopita," alisema Patrick.

Naye Kocha Mkuu, Patrick Aussems alimshukuru mwekezaji huyo kutimiza ahadi aliyokuwa amewaahidi msimu uliopita, na kudai itawasaidia wachezaji kujituma zaidi.

"Nashukuru mwekezaji kutimiza ahadi aliyotuahidi msimu uliopita itazidi kutupa morali ya kufanya vizuri," alisema.

Katika hatua nyingine Mo Dewji amemteua aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu, Crescentius Magori kuwa Mshauri Binafsi wa Mwenyekiti wa Bodi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >